



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI


RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABUZA SERIKALI

**KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA
MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA
FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2012**

Machi, 2013



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam. Simu ya Upepo:
'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
Dar es Salaam.

**Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa
Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Taarifa za Fedha za
Miradi ya Maendeleo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni,
2012**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti ya kwanza inayohusu miradi ya maendeleo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 iliyotajwa hapo juu.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

YALIYOMO

Vifupisho	vi
Dibaji.....	x
SHUKRANI	xiii
SURA YA KWANZA	1
1.0 UTANGULIZI.....	1
1.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Miradi inayofadhiliwa na Washirika wa maendeleo.....	1
1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Miradi ya Maendeleo.	2
1.3 Muundo wa Kazi za Ukaguzi	2
Majukumu na Maslahi ya Watumishi	2
1.4 Mawanda na Viwango vya Ukaguzi vinavyotumika.....	4
1.4.1 Mawanda ya Ukaguzi	4
1.4.2 Viwango vya Ukaguzi Vinavyotumika.....	4
1.5 Sera ya Kihisibu.....	5
1.6 Kuandaa na Kuwasilisha Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi	5
1.6.1 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na.....	5
Sekretarieti za Miko.....	5
1.6.2 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.....	5
1.7 Mfumo wa Udhhibiti wa Ndani.....	6
SURA YA PILI	7
MISINGI NA MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI.....	7
2.0 Utangulizi	7
2.1 Aina ya Hati ya Ukaguzi	7
2.2 Mwelekeo wa hati za ukaguzi	9
SURA YA TATU.....	14
UTENDAJI WA KIFEDHA.....	14
3.0 Utangulizi	14
3.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.....	14
3.2 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).....	17

3.3.0 Programu ya Maendeleo Katika Sekta ya Kilimo	20
3.4 Ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Afy.....	24
3.5 Miradi Mingine	28
SURA YA NNE	36
UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UKAGUZI	36
4.0 Utangulizi	36
4.1 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).....	37
4.2 Programu ya Maendeleo ya Sekta Ya Kilimo	57
4.3 Mfuko wa Maendeleo ya Afya	86
4.4 Progamu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.....	126
4.4.1 Utangulizi	126
4.5 Miradi Mingine ya Maendeleo.....	152
SURA YA TANO.....	163
MAPITIO YA TARATIBU NA MIKATABA YA MANUNUZI.....	163
5.0 Utangulizi	163
5.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo	163
5.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya	165
5.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).....	167
5.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.....	169
5.5 Miradi mingine	174
SURA YA SITA	177
UDHAIFU KATIKA USIMAMIZI WA FEDHA.....	177
6.0 Utangulizi	177
6.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)	177
6.2 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji	180
6.3 Mfuko wa Maendeleo ya Afya	186
6.4 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF)	188

6.5	Mfuko wa Kimataifa wa kupamba na UKIMWI, Malaria, kifua kikuu na Ukoma	192
	SURA YA SABA	199
	HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	199
7.1	Hitimisho	199
7.2	Mapendekezo	202
	VIAMBATISHO	204

Vifupisho

A/C	Akaunti
ACGEN	Mhasibu Mkuu wa Serikali
ASDP	Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
ASDS	Mkakati wa maendeleo ya Sekta ya umma
ASLMS	Wizara zinazojihusisha katika sekta ya Kilimo
BoQ	Mchanganuo wa gharama za kazi za ujenzi
BWOs	Ofisi za mabonde ya Maji
CAATs	Mbinu za ukaguzi zinazotekelezwa kwa kutumia Tekinolojia ya komputa.
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CDTI	Chuo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii
CFS	Taarifa Jumuifu za fedha
CMC	Kamati ya Ugozi wa Jamii
CPO	Ofisi Kuu ya Malipo
DADPs	Mipango ya Maendeleo ya Kilimo katika Wilaya
DANIDA	Shirika la kimataifa la Maendeleo la Denmark
DDPs	Mipango ya Maendeleo ya Wilaya
DSS	Kitengo cha Uchunguzi wa tiba
EU	Jumuia ya Umoja wa Ulaya
HBF	Mfuko wa Uchangiaji Sekta ya Afya
IA	Shirikira la Msaada la Nchi ya Ireland
IDA	Shirika la kimataifa la Maendeleo
IFAD	Mfuko wa kimataifa kwa Maendeleo ya Kilimo
ISA	Viwango vya kimataifa vya ukaguzi
ISSAIs	Viwango vya kimataifa vya ukaguzi vya Ofisi za ukaguzi wa Umma
JICA	Shirika la Maendeleo la nchi ya Japan
LAFM	Mwongozo wa Uhasibu wa Serikali za Mitaa
LGAs	Mamlaka za Serikali za Mitaa
MDAs	Wizara, Idara na Wakala
MDG	Malengo ya Maendeleo ya Milenia
MoU	Mkataba wa Makubaliano
MoW	Wizara ya Maji
NAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
NBAA	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na wakaguzi wa hesabu
NVF	Mfuko wa Taifa wa Fedha kwa ajili ya Vijiji
NWSDS	Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Maji
PFA	Sheria ya fedha za umma no6 ya 2001

	(kama ilivyorekebishwa 2004)
PFGAs	Vikundi shirikishi vya wakulima.
PFMRP	Mradi wa maboresho ya usimamizi wa fedha za umma
PFR	Kanuni za fedha za umma
PMG	Mlipaji mkuu wa serikali
PPA	Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004
PPRA	Mamlaka ya kusimamia Ununuzi wa umma
RWBO	Shirika la maji la bonde la Rufiji
Sect.	Kifungu
SIDA	Shirika la kimataifa la maendeleo la Sweden
SNAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden
TASAF	Mfuko wa Maendeleo ya jamii Tanzania
TMU	Kitengo cha Uongozi wa Mfuko wa Maendeleo Jamii
TPRS	Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
URT	Jamhuri ya Muugano wa Tanzania
USD	Dola ya Kimarekani
VFC	Mratibu wa Fedha wa Kijiji
WSDP	Programu ya maendeleo ya sekta ya maji
MSD	Bohari kuu ya madawa.
NIMR	Kitengo cha utafiti wa magonjwa
G-TZ	Ushirikiano wa Tanzania na Ujerumani
INTOSAI	Tasisi ya kimataifa inayojumuisha Asasi kuuza Ukaguzi Kimaifa
AFROSAI - E	Tasisi inayojumuisha ofisi za ukaguzi za nchi za kiafrika zinazozungumza lugha ya kigereza

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**(Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri
ya Muungano wa Tanzania)**

Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Dira

Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma.

Dhamiri

Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

- **Uadilifu**
Sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.
- **Ubora**
Sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi.
- **Uaminifu**
Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa Sheria.
- **Mtazamo wa watu**
Tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
- **Uvumbuzi:**
Sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.
- **Matumizi bora ya rasilimali**
Sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

Tunatimiza haya kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuchangia katika matumizi bora ya fedha za umma kwa kuhakikisha kwamba wakaguliwa wetu wanawajibika kutunza rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuimarisha ubora wa utoaji huduma kwa kuchangia ubunifu kwa matumizi bora ya rasilimali za umma;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau wetu kuhusu mapungufu katika uendeshaji wa shughuli zao;
- Kuwahusisha wadau wetu katika mfumo wa ukaguzi; na
- Kuwapa wakaguzi nyenzo za kufanya kazi ambazo zitaimarisha uhuru wa ofisi ya ukaguzi.

© Ripoti hii imekusudiwa kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali. Hata hivyo, mara baada ya kupokelewa na Spika na kuwasilishwa Bungeni, ripoti hii huwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hauwezi kuziwa.

Dibaji

Ripoti hii ni majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa miradi inayofadhiliwa na wahisani na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miradi ipo katika makundi mawili ambayo ni miradi mikubwa minne na mingine kama inavyoonekana hapa chini:

- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(TASAF)
- Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)
- Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP)
- Mfuko wa Sekta ya Afya (HBF)

Pamoja na ukaguzi wa miradi ambayo washirika wa maendeleo wanachangia kwa pamoja (Basket Funds), pia nilikagua miradi mingine ambayo ni makubaliano kati ya Serikali na wahisani wengine.

Ripoti hii ya Ukaguzi inawasilishwa kwa Mheshimiwa Raisi kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu 34(1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Kwa mujibu wa Ibara 143 (2) (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Ibara ya 143(4) inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha kwa Mheshimiwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ripoti yoyote anayotayarisha kuhusu hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha Katiba. Mara baada ya kuipokea ripoti hiyo, Mheshimiwa Raisi ataagiza ripoti iwasilishwe Bungeni ambapo inapendekezwa iwe siku saba kabla ya kumalizika kwa kikao cha Bunge.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa Ofisi yangu katika kutimiza jukumu lake Kikatiba. Haya ni matokeo ya jitihada za Mheshimiwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge letu tukufu.

Uhuru wa kiutendaji utaniwezesha kudhibiti rasilimali za ofisi zilizopo zikihusisha rasilimali watu na fedha zitakazowezesha ofisi yangu kutimiza majukumu yake bila kuingiliwa na Mamlaka yoyote.

Sheria imeongeza mawanda ya ukaguzi wetu kwa kunipa madaraka ya kufanya kaguzi nyingine zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha ambazo ni ukaguzi wa ufanisi, utambuzi na mazingira na kaguzi maalum. Ni matumaini yangu kwamba, kwa kuanzishwa kwa Sheria mpya ya Ukaguzi wa Umma, Ofisi yangu itaweza kuimarisha udhibiti wa fedha na kuisaidia Serikali kuimarisha uwajibikaji. Kwa hiyo, Sheria inaniwezesha kuwa huru na kulihakikishia Bunge masuala yanayohusu uwajibikaji, uwazi na matumizi bora ya rasilimali hasa kuona kwamba rasilimali hizo zimetumika vizuri kwa kuzingatia uchumi, ufanisi na kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge.

Ni vyema kutambua kuwa wakati ofisi yangu inatoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa Sheria, taratibu na kanuni mbalimbali na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye taasisi za Umma na hasa miradi ya maendeleo, wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani ni jukumu la Maafisa Masuuli.

Matarajio ya Bunge na umma ni kuona kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi watahakikisha utoaji wa taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali katika miradi ya maendeleo kuhusiana na ufanisi, ubora na usimamizi wa mipango iliyowekwa. Kwa njia ya ukaguzi, ofisi inachangia katika kutoa mapendekezo kuhusu uimarishaji na uboreshaji wa sekta ya Umma. Kwa msingi huu, Serikali Kuu na Ofisi yangu na

washirika wa maendeleo wana mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa umma katika usimamizi wa rasilimali za Umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora ya rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge nayale ya umma kwa mapana zaidi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya umma inayopokea fedha toka kwa washirika wa maendeleo. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia katika usimamizi fedha katika sekta ya umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tunaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa fedha zinazotolewa na washirika wa maendeleo na utoaji wa huduma bora kwa Watanzania.

Hivyo, nitafurahi kupata taarifa ya jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu hii kwa siku zijazo.



Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Dar es Salaam,

Marchi, 2013

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani kwa wote walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba.

Natoa shukrani za dhati kwa wadau wetu ambao ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, Hazina, pamoja na Maafisa Masuuli wote wa Wizara (MDAs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) wanaosimamia miradi inayofadhiliwa na Wahisani kwa kutoa ushirikiano na kutoa taarifa muhimu zinazohitajika sana katika utayarishaji wa ripoti hii.

Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupita Shirika la Kimataifa la Misaada la Maendeleo la Sida, Benki ya Dunia kupita Mradi wa Kusimamia na Kuboresha Sekta ya Fedha za Umma (PFMRP) na wote wenye mapenzi mema ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha Ofisi yangu. Mchango wao umekuwa na manufaa makubwa katika kuendeleza na kukuza rasilimali watu, nyezo za kazi (magari), mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na vitendea kazi. Bado tunahitaji msaada zaidi katika kuboresha ukaguzi katika sekta ya umma ambao ungeweza kuharakishwa kama tungepata wafadhili wenye nia ya kutoa fedha za ujenzi wa chuo cha mafunzo ya ukaguzi kinachotarajiwa kujengwa Gezaulole-Kigamboni.

Aidha, nawashukuru watumishi wote wa umma popote pale walipo hapa Tanzania wawe ni wa Serikali Kuu au Serikali za Mitaa bila ya kuwasahau walipa kodi ambao ndio walengwa wa ripoti hii. Michango yao imekuwa msaada mkubwa katika ujenzi wa Taifa ambao hauwezi kupuuzwa hata kidogo.

Ninapenda kutambua utaalamu na kujituma kwa watumishi wa Ofisi yangu katikakufikia malengo ya kazi yaliyowekwa ingawa walitimiza hayo katika mazingira magumu yakiwemo ukosefu wa fedha, vitendea kazi,

mishahara midogo na kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikiwa kirahisi.

Napenda kutoa shukrani kwa wote walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba. Kwa mara nyingine, napenda kutoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wote wa Ofisi yangu kwa kuniwezesha kutoa ripoti hii kwa wakati. Ninawajibika kutoa shukrani zangu za pekee kwa familia yangu na familia za wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa kutuvumilia kwa kutokuwa nao kwa muda mrefu wakati tukikamilisha majukumu haya ya kikatiba.

Mwisho, natoa shukrani zangu kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuniwezesha kutoa ripoti kwa wakati.

Naomba Mungu awabariki wote wakati tukitimiza wajibu wetu katika uwajibikaji na utawala bora kwa kutumia vyema rasilimali za umma.

MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA MIRADI INAYOFADHILIWA NA WASHIRIKA WA MAENDELEO KWA MWAKA 2011/2012

Ripoti hii ya miradi inayofadhiliwa na washiriki wa mendeleo imegawanyika katika maeneo yafuatayo:

- A. Utangulizi
- B. Hati za ukaguzi zilizotolewa
- C. Uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi pamoja na utendaji wa miradi mikubwa na miradi mingine
- D. Mapungufu katika mchakato wa manunuzi
- E. Usimamizi wa fedha na mali
- F. Tathmini ya utendaji wa miradi mikubwa na miradi mingine.
- G. Hitimisho na mapendekezo

A: Utangulizi

Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha katika miradi inayofadhiliwa na Washirika wa maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. Mawanda ya ukaguzi katika miradi inayofadhiliwa na wahisani yanajumuisha Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP), Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mfuko wa Uchangiaji wa Sekta ya Afya (HBF) na miradi mingine.

B: Utoaji wa Hati za Ukaguzi

Matokeo ya ukaguzi wa miradi inayofadhiliwa na wahisani kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 ni kama yanavyoonekana katika jedwali namba 1 hapa chini:-

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa hati za Hati ya ukaguzi zilizotolewa

Maelezo	Hati zinaziridhisha bila maswala ya msisitizo	Hati zinaziridhisha na maswala ya msisitizo	Hati zenye Shaka	Hati zisizoridhis ha	Hati mbaya	Jumla
TASAF	28	75	24	0	0	127
ASDP	17	82	33	0	0	132
WSDP	10	95	25	1	0	131
HBF	6	94	32	0	0	132
Jumla ndogo	61	346	114	1	0	522
Miradi mingine	68	22	3	0	0	93
Jumla Kuu	129	368	117	1	0	615

C: Ripoti Kuhusu Tathmini ya Ufanisi wa Miradi Inayofadhiliwana Wahisani

Sehemu hii inatoa kwa ufupi taarifa ya utendaji na ufanisi wa miradi mikubwa ikiwemo vyanzo vya fedha, matumizi ya fedha na bakaa ya fedha ambazo hazikutumika hadi tarehe ya kufunga hesabu. Katika mwaka huu wa ukaguzi, nimeonyesha uchambuzi kuhusu ufanisi wa miradi ili kupima na kuona kama fedha zilizopelekwa katika miradi hiyo zimetumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kama pamekuwepo mchango kwenye uchumi wa nchi ikihusisha maendeleo ya jamii, changamoto zilizopatikana na kama thamani ya fedha ilipatikana.

D: Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Sura hii inaonyesha mambo yaliyosababisha utoaji wa aina fulani ya hati za ukaguzi kwa miradi ya maendeleo. Uchambuzi huu unakusudia kuainisha vigezo vilivyotumika kutoa hati za ukaguzi ambazo zimejadiliwa katika sura inayofuata.

Miradi minne (4) inayofadhiliwa na Wahisani ilikaguliwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 ambapo miradi mingine tisini na tatu (93) ilikaguliwa na kufanya jumla ya miradi iliyokaguliwa kuwa tisini na saba (97)

E: Kasoro Katika Manunuzi

Katika barua nilizowasilisha kwa Maafisa Masuuli, nilitoa taarifa kwamba, miradi mingi inayofadhiliwa na wahisani ilikuwa na kasoro nyingi katika manunuzi zilizokiuka Sheria ya Manunuzi Na. 21 ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005. Mapitio ya mchakato wa manunuzi yanaonyesha kwamba kuna kutozingatia Sheria na kanuni za manunuzi, hivyo inapendekezwa pawepo na kuzingatia Sheria na kanuni wakati wa kufanya manunuzi.

G: Hitimisho na Mapendekezo

Mwisho, kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008, nimetoa mapendekezo kwenye sura ya saba(7)ya ripoti hii, ambayo kama yatatekelezwa, ninaamini yataongeza ufanisi katika usimamizi wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani nchini. Mapendekezo ninayotoa ni kama ifuatavyo.

- Ukaguzi wa ndani katika Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa hauridhishi kutokana na kutokaguliwa maeneo muhimu kama ukaguzi wa taarifa za fedha na shughuli za miradi inayofadhiliwa na wahisani wa maendeleo katika eneo muhimu la uwajibikaji na tathmini ya utendaji wa miradi kwa mujibu wa mkataba wa maelewano(MoU).
- Kutokana na ukweli kwamba utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo hufanywa na watendaji wa ngazi za chini katika vijiji, maafisa masuuli katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hawapati muda wa kutosha wa kusimamia miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo.
- Maafisa masuuli hawatoi umuhimu wa kutosha wa kushughulikia mapendekezo na maswala yaliyohojiwa na wakaguzi. Hii inatokana na ushahidi kwamba,palikuwepo na mapendekezo yasiyojibiwa ya kipindi kilichopita ya Sh.20,289,040,011.

- Ripoti hii imeonyesha kwamba, mfuko wa maendeleo ya afya ulikuwa na maswala yasiyojibiwa yenye thamani ya Sh. 10,982,257,870, ikifuatiwa na mfuko wa maendeleo ya kilimo ya sh. 9,086,703, 966 na mwisho ni mfuko wa maendeleo ya maji ukiwa na maswala yasiyojibiwa ya Sh. 220,078,175.
- Pamekuwepo na ucheleweshwaji wa fedha toka kwa washirika wa maendeleo na Hazina kwenda kwa watekelezaji wa miradi. Ucheleweshaji huu wa fedha umesababisha kuchelewa au kutokutekelezwa kwa miradi iliyokusudiwa na pia kuwepo na kiasi kikubwa cha fedha kisichotumika cha Sh. 299,852,509,319, na Dola za Marekani 213,520,573 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012.
- Kumekuwepo na malipo yasiyostahili ya Sh. 1,617,109,102 ambapo kiasi cha sh. 1,036,474,688 kilitumika katika mradi wa maendeleo ya kilimo, Sh. 353,036,793 kilitumika katika mradi wa maendeleo ya maji na Sh. 227,597,621 kilitumika katika miradi mingine. Kuwepo kwa matumizi yasiyostahili kunadhihirisha kwamba Maafisa masuuli walitumia fedha za miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa matumizi yasiyostahili.
- Tuligundua udhaifu uliokithiri wa usimamizi wa miradi kwa ujumla ambapo katika mwaka 2011/2012, palikuwepo na malipo yaliyofanywa bila kuwa na viambatisho muhimu ya sh. 1,264,915,933 katika Halmashauri tisa (9) kinyume cha kifungu cha 34(1) cha Memoranda ya uhasibu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 na mwongozo wa uhasibu wa mwaka 2009 aya ya 2.4.1.
- Kulikuwepo na malipo yasiyokuwa na hati za malipo ya Sh. 730,967,490. Mradi wa maendeleo ya kilimo ulikuwa na malipo yasiyokuwa na hati za malipo ya

Sh. 320,062,215 ukifuatiwa na mfuko wa maendeleo ya Afya ukiwa na malipo ya Sh. 296,087,278, mfuko wa maendeleo ya jamii ukiwa na malipo ya Sh. 71,010,497 na miradi mingine ikiwa na malipo ya Sh. 43,807,500 .Malipo haya yalikiuka kifungu cha 34(1) cha Memoranda ya Uhasibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

- Maafisa masuuli wa Halmashauri kumi na sita(16) walikiuka kanuni ya ununuzi wa umma Na.68 (5) (Mali,Kazi ,huduma zisizo za ushauri pamoja na uuzaji wa mali za umma kwa njia ya mnada kwa kuzingatia kanuni ya mwaka 2005 pamoja na kitungu Na.272 cha Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na Memoranda ya makubaliano kwa kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka kwa wauzaji mbalimbali zenye thamani ya Sh. 291,928,527 bila idhini ya Bodi za Zabuni.
- Malipo ya Sh. 305,125,078 yalilipwa kwa wauzaji mbalimbali wa bidhaa kabla mapokezi ya bidhaa hizo kufanyika.Hata hivyo,ukaguzi uligundua kuwa mapokezi ya bidhaa hizo hayakuthibitishwa na kukiuka kifungu Na. 71(1) (b) cha sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Vifaa vya utabibu venye thamani ya Sh.412,219,600 vilinunuliwa katika Halmashauri tisa (9) kutoka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bohari ya madawa na kukiuka kifungu cha 4 cha kanuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa,(uanzishwaji wa Bodi za Zabuni) kanuni ya mwaka 2007.
- Wizara ya fedha inapaswa kuimarisha Idara ya ukaguzi wa ndani kwa kutoa mwongozo thabiti kwa Maafisa masuuli katika kuimarisha uhibititi wa ndani na kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za Serikal.

- Aidha, Wizara inapaswa kuhakikisha kwamba Maafisa masuuli wote wanaandaa taarifa za fedha na kuziwasilisha kwa ukaguzi kwa wakati. Kuna haja kwa Wizara kutoa adhabu kwa Maafisa masuuli wataoshindwa kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa.
- Washirika wa maendeleo, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa wahakikishe utoaji wa fedha kwa wakati kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyoainishwa kutekelezwa na kuepuka miradi kubakiwa na kiasi kikubwa cha fedha zisizotumika wakati wa kufunga mwaka.
- Maafisa masuuli ambao ni wahusika katika usimamizi wa miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo waongeze juhudi za kujibu mapendekezo ya ukaguzi uliopita ili kuepuka kurudiwa kwa maswala yaliyokwisha kuhojiwa kipindi kijacho.
- Maafisa masuuli wahakikishe kwamba kunakuwepo na gharama ndogo na thamani ya fedha zilizotumika wakati wa kupanga, kuainisha mradi na utekelezaji wa miradi.
- Maafisa masuuli wanapaswa kuhakikisha kwamba, matumizi ya fedha katika ununuzi wa kazi za ujenzi, ununuzi wa bidhaa na huduma yanazingatia matakwa ya sheria ya ununuzi wa umma ya mwaka 2004 pamoja na kanuni zake za mwaka 2005 pamoja na kifungu Na.272 cha Memoranda ya fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na Memoranda za makubaliano ili kuepuka manunuzi yasiyo ya lazima.
- Washirika wa maendeleo wanaombwa kutenga bajeti ya fedha za kugharimia ukaguzi wa miradi mikubwa kutokana na ukweli kwamba utoaji wa fedha kutoka Hazina na Washirika wa maendeleo

kugarimia ukaguzi wa miradi hiyo hazipokelewi kwa wakati na uhakika.

- Kutokana na ukaguzi uliofanywa, na matokeo yaliyopatikana, miradi na programu zinazokabidhiwa na kusimamiwa na wananchi wenyewe, imeonyesha maendeleo mazuri na kudumu. Matokeo haya ni sahihi kwa kuchukua mfano wa Mfuko wa maendeleo ya jamii ambao unamilikiwa na wananchi na unaendelea vyema kutoa huduma kwa jamii.
- Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMlinapaswa kusimamia miradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kwamba inatekekezwa kwa mujibu wa memoranda ya maelewano. Kwa mfano, utayarishaji wa taarifa za fedha na ukaguzi ni matakwa ya msingi.
- Serikali inapaswa kutathmini sifa za watumishi kwenye mamlaka za Serikali za mitaa kwani kuna ushahidi kwamba kuna uhaba mkubwa wa watumishi wenye sifa za kusimamia shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo.
- Katika ripoti yangu ya mwaka uliopita, nilieleza kwamba, ukaguzi wa miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo ambayo ni Mradi wa maendeleo ya kilimo, mfuko wa maendeleo ya Afya, mfuko wa maendeleo ya jamii na miradi mingine ulikuwa na changamoto kwa Ofisi yangu kutokana na kukosekana kwa Wakaguzi wa kutosha pamoja na ukosefu wa fedha. Katika mwaka huu wa fedha ofisi yangu imekabiliwa na matatizo yaliyojitokeza mwaka uliopita. Ni wazi kwamba, ukaguzi wa baadhi ya miradi iliyotajwa hapo juu utafanywa na wakaguzi wakujitegemea kwa niaba yangu, lakini jukumu la kutoa ripoti za ukaguzi litabaki kuwa la ofisi yangu.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Ripoti hii inatolewa kwa mara ya pili kufuatia ukaguzi wa hesabu na nyaraka nyingine za miradi inayofadhiliwa na Washirika wa maendeleo kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebisha 2005) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Aidha kwa miaka mingi ya nyuma, ofisi yangu ilikuwa ikifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa kutoa barua na ripoti za ukaguzi kwa Maafisa Masuuli. Hivyo masuala ya miaka ya nyuma yasiyoshughulikiwa yanahusu taarifa za ukaguzi nilizotoa kwa kila Afisa Masuuli anayehusika na miradi.

1.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Miradi inayofadhiliwa na Washirika wa maendeleo

Kutokana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninapaswa kukagua kumbukumbu za taarifa zote za hesabu za fedha katika ofisi zote za Umma, Mahakama na Mamlaka zote za Serikali ya Muungano wa Tanzania ikiwamo miradi ya maendeleo kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Raisi ambaye atahakikisha zinawasilishwa mbele ya Bunge.

Katika kutimiza wajibu huu, kutokana na Kifungu Na.10 cha Sheria Na 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ninatakiwa kujiridhisha kwamba:-

- Tahadhari inachukuliwa ili kuhakikisha kwamba fedha za miradi ya maendeleo zinakusanywa na kutunzwa kwa mujibu wa Sheria na miongozo iliyowekwa.
- Fedha zote zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinatumika kulingana na matumizi yaliyokusudiwa na kwa mujibu wa Sheria na kanuni

za fedha na ugavi pamoja na makubaliano na wafadhili.

Aidha, kutokana na Kifungu kilichotajwa hapo juu ninawajibika kumtanabaisha Rais na Bunge juu ya uwepo wa matumizi mabaya ya fedha na mali za Umma.

1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Miradi ya Maendeleo.

Wajibu wangu kama Mkaguzi Mkuu ni kutoa hati ya ukaguzi kuhusu hesabu za fedha zilizoandaliwa. Nilikagua kulingana na viwango vya kimataifa vya ukaguzi viwango vya kimataifa vinavyosimamia ukaguzi (ISA) katika taasisi za umma za Ukaguzi (ISSAls) na taratibu nyingine nilizoona zinafaa.

Zaidi ya hayo, imebainishwa chini ya Kifungu Na 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Kutokana na Sheria hiyo, ninawajibika kuchunguza, kukagua na kutoa taarifa juu ya hesabu za Wizara na Idara za Serikali na Maafisa Masuuli, na watu wote waliokabidhiwa jukumu la kukusanya, kupokea, kutunza, kutoa au kuuza, kuhamisha na kutoa stakabadhi, dhamana, vifaa au mali nyingine za Umma. Pia, jukumu langu linahusu Mashirika yote ya Umma na Taasisi nyingine, Mamlaka yoyote au Taasisi inayopokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali au Taasisi yoyote ambayo imeruhusiwa kisheria kukaguliwa na Ofisi yangu.

1.3 Muundo wa Kazi za Ukaguzi

Ripoti hii inatoa kwa muhtasari matokeo ya mwisho ya zoezi la ukaguzi ambalo lilifanywa na Ofisi yangu nchini kote katika mwaka huu. Ili Ofisi yangu iweze kushughulikia kikamilifu kazi hii kubwa ya kukagua miradi ya maendeleo, kuna Ofisi katika Wizara na Mikoa yote Tanzania Bara ili kurahisisha utendaji.

Majukumu na Maslahi ya Watumishi

Majukumu ya Ofisi yangu yameongezeka kwa kiwango kikubwa yakilinganishwa na miaka ya nyuma.

Majukumu yamekuwa makubwa zaidi baada ya madaraka ya kifedha kwenda hadi ngazi ya Tarafa, vijiji na hivyo kuwepo na haja ya msingi ya Ofisi yangu kuwa na matawi ngazi ya Wilaya. Pamoja na kuongezeka kwa wigo na ukubwa wa majukumu, uwezo wa kifedha na maslahi kwa watumishi yamekuwa madogo.

Ningependa kutambua juhudi za Serikali katika kuboresha hali za wafanyakazi katika Ofisi yangu ijapokuwa juhudi zaidi zinatakiwa kuboresha maslahi hayo yaendane na mazingira halisi ya kazi inayofanywa. Nimewasilisha mapendekezo ya muundo mpya wa Ofisi yangu ambao umepitishwa na Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Februari 2010. Juhudi za kuanza kutumia muundo huu zinaendelea; hii ni pamoja na kutoa mafunzo ya taaluma ya uhasibu ili kupata watumishi wenye sifa stahiki kujaza nafasi zilizopo. Pia, nimewasilisha mapendekezo ya mishahara katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa watumishi wa Ofisi yangu miaka miwili iliyopita.

Mapendekezo hayo yalikataliwa kwa maelezo kuwa marekebisho ya mishahara yaliyofanywa kwa watumishiwa sekta ya umma yaliwahusu pia watumishi wa ofisi yangu.

Kwa sasa ofisi yangu imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kiasi kikubwa. Nia ya ofisi ni kupanua ofisi za ukaguzi hadi ngazi ya wilaya ambako fedha nyingi za maendeleo zinaelekezwa na Serikali na Wafadhili. Juhudi hizi zitahitaji Serikali kuridhia maombi ya mapendekezo ya marekebisho ya mishahara pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya upanuzi wa mawanda ya ukaguzi unaokusudiwa.

Pia ni nia yangu kuhakikisha kwamba wakaguzi wanafundishwa mbinu mbalimbali za ukaguzi ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa mazingira, jinsia, ukaguzi wa mifumo ya teknolojia ya kisasa, (mbinu za ukaguzi

zinazotekelezwa kwa kutumia teknolojia ya kompyuta - CAATs).

1.4 Mawanda na Viwango vya Ukaguzi vinavyotumika

1.4.1 Mawanda ya Ukaguzi

Mawanda ya ukaguzi kwa kifupi yanahusisha upokeaji wa fedha za Wahisani, uidhinishaji wa matumizi kwa kufuata sheria na makubaliano na Wafadhili katika utekelezaji wa miradi. Ukaguzi ulifanyika ili kujiridhisha kwamba kulikuwepo na uzingatiaji wa kanuni zilizopo, kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji na kubainisha kasoro zilizojitokeza, ingawaje siyo zote.

Wakati wa ukaguzi, Maafisa Masuuli wanataarifiwa kuhusu hoja zilizojitokeza na kupewa muda wa kujibu hoja hizo. Maafisa Masuuli wanapewa fursa ya kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza mapendekezo mbalimbali na maoni ya ukaguzi. Barua ya ukaguzi ni kwa ajili ya hoja mbalimbali pamoja na ushauri kwa Afisa Masuuli mhusika na ripoti inapelekwa kwa vyombo vinavyowasimamia Maafisa Masuuli na Umma kwa ujumla.

1.4.2 Viwango vya Ukaguzi Vinavyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ni mwanachama wa Taasisi ya Kimataifa inayojumuisha Asasi Kuu za Ukaguzi Kimataifa (INTOSAI). Pia Ofisi ni mshirika wa Taasisi inayojumuisha Ofisi za Ukaguzi za nchi za Kiafrika zinazozungumza lugha ya Kiingereza (AFROSAL -E). Hivyo, Ofisi inatumia Viwango vya Ukaguzi vya ISSAI pamoja na Viwango vya Kimataifa (ISA) vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC). Viwango hivi vinanitaka kuzingatia maadili katika kuandaa mipango ya ukaguzi na kukagua ili kupata uhakika wa taarifa za fedha na kubaini madhaifu yaliyomo.

1.5 Sera ya Kihhasibu

Taarifa za fedha za miradi ya maendeleo hutayarishwa kulingana na makubaliano yaliyotiwa saina, pia mifumo ya usimamizi wa fedha za umma nchini huzingatiwa.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 53 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004), Serikali imeweka taratibu za kihhasibu ili kuhakikisha kwamba rasilimali zinazoidhinishwa na Bunge zinatumiwa kwa usahihi. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004), Maafisa Masuuli wanapaswa kuhakikisha kwamba mapato yote ya Umma yanaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia malipo kutoka kwenye Mfuko huo yataidhinishwa kwa Sheria ya Bunge ya Matumizi kwa mwaka husika.

1.6 Kuandaa na Kuwasilisha Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

1.6.1 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa

Maafisa Masuuli ni wasimamizi wa rasilimali za Umma kwenye maeneo yao ya kazi kulingana na matakwa ya Kifungu Na.25(4)cha Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004). Katika kulinda rasilimali zilizo chini yao, suala la kuweka mifumo madhubuti na udhibiti wa ndani ni la umuhimu mkubwa. Ni wajibu wa uongozi wa halmashauri kuhakikisha kwamba kumbukumbu za kihhasibu za miradi zinatunzwa vizuri na kutoa uhakika wa taarifa za fedha na kulinda na kuhifadhi mali zote.

1.6.2 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Pale ambapo halmashauri inapokea fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo, zinakuwa na Jukumu la kutayarisha taarifa za fedha, kama ulivyofafanuliwa katika Agizo namba 53 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Washirika wa maendeleo na Serikali.

Agizo Na.9 16 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 inaelekeza Halmashauri kuweka

mfumo wa udhibiti wa ndani wa rasilimali za Serikali ikiwa ni pamoja na fedha za miradi ya Maendeleo. Vile vile agizo namba 53 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linaelekeza Hesabu ziandaliwe kufuata na sheria, kanuni, na maendeleo yanayotolewa na Waziri husika na TAMISEMI, na viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu (IPSAS).

1.7 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Udhibiti wa ndani unamaanisha namna zote ambazo rasilimali za Serikali zinaelekezwa, zinasimamiwa na kupimwa. Udhibiti wa ndani unayo nafasi kubwa katika kuzuia na kugundua ubadhirifu/matumizi mabaya na kulinda rasilimali za Umma zilizo dhahiri na zisizo dhahiri.

Kuweka na kusimamia mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani ni jukumu la uongozi/menegimenti ya taasisi husika.

SURA YA PILI

MISINGI NA MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI

2.0 Utangulizi

Lengo kuu la kufanya kaguzi mbalimbali ni kutoa maoni huru ya kitaalamu kama taarifa za fedha zinaonesha hali halisi ya kifedha ya mkaguliwa. Hati hii hutolewa ili kumwezesha mtumiaji wa taarifa za fedha kama hakikisho ili aweze kufikia maamuzi kutokana na matokeo ya ukaguzi uliofanywa.

Inakusudia kulishauri Bunge na watumiaji wengine wa taarifa za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kama taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango kubalifu vya Kimataifa vya kutayarisha taarifa za fedha katika sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 25 (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (ilivyorkebishwa 2004) ikiwemo Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizowekwa.

Ni muhimu kutambua kwamba hati ya ukaguzi inayotolewa kwa taarifa za fedha siyo hakikisho la moja kwa moja kwamba hali ya kifedha ya taasisi ni nzuri na sahihi kabisa kuweza kutegemewa katika kufanyia maamuzi. Hati ya ukaguzi ni maoni tu kwamba taarifa iliyowasilishwa ni sahihi na haina makosa makubwa ambapo maamuzi mengine huachiwa mtumiaji wa taarifa kuamua.

2.1 Aina ya Hati ya Ukaguzi

Kuna aina tano (5) za hati za ukaguzi, kila moja ikieleza mazingira tofauti anayokutana nayo mkaguzi. Hati hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Hati inayoridhisha

Wakati mwingine hati hii huchukuliwa na wengi kama “hati safi”. Aina hii ya hati hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa zinakuwa hazina makosa mengi na zimezingatia matakwa ya viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa mujibu wa KifunguNa. 25 (4) cha Sheria ya Fedha za

Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha 2004) ikihusisha uzingatiaji wa Sheria na Kanuni.

(ii) Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo

Katika mazingira fulani, hati ya ukaguzi inayoridhisha huweza kurekebisha kwa kuongeza aya yenye masuala ya msisitizo yanayodokeza masuala muhimu ambayo yasiporekebisha na mkaguzi yanaweza kusababisha kutolewa kwa hati yenye shaka katika ukaguzi unaofuata.

Kuongezwa kwa aya ya masuala ya msisitizo hakuathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa.

Madhumuni ya masuala ya msisitizo ni kutoa uelewa zaidi kwa hali iliyotokea wakati wa ukaguzi licha ya kutolewa kwa hati ya ukaguzi inayoridhisha.

(iii) Hati yenye Shaka

Hali na mazingira inayosababisha kutolewa kwa hati hii, huwa katika kundi moja au mawili ambayo ni:

- Kunapokuwa na mashaka juu ya jambo fulani husababisha mkaguzi ashindwe kutoa maoni juu ya ukaguzi.
- Pale ambapo mkaguzi anapotoa maoni yanayotofautiana na hali halisi ya taarifa ya fedha zilizotolewa (kutokubaliana na taratibu kubalifu za utunzaji na uzingatiaji wa Sheria na kanuni).

Kwa hali hiyo, hati yenye Shaka inaonyesha kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa ni sahihi isipokuwa kwa madhara yatokanayo na masuala halisi ya kiukaguzi yaliyogunduliwa.

(iv) Hati Isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha hutolewa inapogundulika kuwa taarifa za fedha za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa kiasi kikubwa si sahihi zinapoangaliwa katika ujumla wake; hazikuandaliwa kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma

(IPSAS) na kwa namna inayotakiwa katika Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha 2004) inayoelezea kuwa taarifa zilizopo siyo sahihi na haziaminiki katika kupima matokeo ya uendeshaji katika Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa.

Maelezo ya hati isiyoridhisha huwa wazi ambapo ninaeleza kwamba taarifa za fedha hazikuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inayotakiwa katika Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (ilyorekebisha 2004).

(v) Hati mbaya

Hati mbaya inaweza kusababishwa na kukosekana kwa uhuru au ufinyu mkubwa wa mawanda ya ukaguzi ama kwa makusudi au la, mkaguliwa kukataa kutoa ushahidi na taarifa kwangu katika maeneo muhimu kwenye taarifa za fedha na panapokuwa na mashaka makubwa katika uendeshaji wa shughuli za mkaguliwa.

2.2 Mwelekeo wa hati za ukaguzi


Jedwalinamba 2 linaonyesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.



Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa hati za maoni ya ukaguzi zilizotolewa


Maelezo	Hati inayoridhisha bila maswala ya msisitizo	Hati inayoridhisha na maswala ya msisitizo	Hati yenye Shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya	Jumla
TASAF	28	75	24	0	0	127
ASDP	17	82	33	0	0	132
WSDP	10	95	25	1	0	131
HBF	6	94	32	0	0	132
Jumla ndogo	61	346	114	1	0	522
Miradi mingine	68	22	3	0	0	93
Jumla Kuu	129	368	117	1	0	615


Maelezo	2011/ 2012	%	2010/ 2011	%
Hati inayoridhisha bila maswala ya msisitizo	129	20.7	273	47
Hati inayoridhisha na maswala ya msisitizo	368	60	211	36.4
Hati yenye Shaka	117	19	92	16
Hati isiyoridhisha	1	.30	2	.30
Hati mbaya	0	0	2	.30
Jumla	615	100	580	100

Taarifa iliyoonyeshwa katika jedwali hapo juu linaweza kuonyeshwa katika chati-mhimili kama ifuatavyo:









SURA YA TATU
UTENDAJI WA KIFEDHA

3.0 Utangulizi

Sura hii inatoa mchanganuo na mwelekeo wa utendaji wa kifedha katika miradi ya maendeleo ikiwemo sekta ya maji, kilimo, afya, maendeleo ya jamii pamoja na miradi mingine ya maendeleo katika kipindi cha 2011/2012.

Miradi hii inafadhiliwa na washirika mbalimbali wa maendeleo ikiwemo serikali ya Tanzania.

3.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

3.1.1 Utendaji wa Kifedha

(a) Akaunti Kuu ya Mradi Hazina

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Serikali ya Tanzania ikishirikiana na washirika wa maendeleo iliwezesha kupatikana kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 52,571,602.65, hata hivyo kulikuwa na bakaa ya kiasi cha Dola za Marekani 14,707,954.93 katika akaunti kuu hivyo kufanya jumla ya Dola za Kimarekani 67,279,557.58 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta hii. Kati ya fedha hizo kiasi cha Dola za Kimarekani 36,581,391.68 kiliamishwa kwenda Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kiasi kingine cha Dola za Kimarekani 963,246.90 kiliamishiwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hivyo kubaki na bakaa ya Dola za Kimarekani 29,734,919 ilipofikia tarehe 30 Juni, 2012 kama ilivyoanishwa katika Jedwali Na.3 hapo chini:

Jedwali Na 3: Utendaji Kifedha katika Akaunti Kuu ya Mradi Hazina

Ufafanuzi	Kiasi kwa Dola za Marekani
Salio la kuanza mwaka 1/7/2011	14,707,954.93
Shirika la msaada la	10,822,712.14

Kijerumani (KFW)	
Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA)	31,510,000.00
Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID)	9,702,000.00
Wizara ya Maji na Umwagiliaji	536,890.51
Jumla ya fedha zilizopatikana	67,279,557.58
Uhamishaji wa Fedha	
Wizara ya Maji na Umwagiliaji	36,581,391.68
Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	963,246.90
Bakaa tarehe 30/06/2012	29,734,919.00

(b) Utendaji wa Kifedha

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kulikuwa na kiasi cha Sh.307,563,235,875kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya maji. Serikali ya Tanzania ikishirikiana na washirika wa maendeleo zilitoa kiasi cha Sh. 295,226,091,899 na kulikuwa na kiasi cha Sh. 24,578,395,400.84ikiwa bakaa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 kama ilivyoanishwa katika Jedwali Na. 4 hapo chini.

Jedwali Na 4: Chanzo cha Fedha za Mradi wa Maji

Serikali ya Tanzania/Wadau wa Maendeleo	Kiasi (Sh.)
Mchango wa Serikali(Tanzania)	26,082,467,232
Wadau wa Mfuko wa Pamoja	181,264,362,674
Wadau wa mifuko mbalimbali	28,495,778,731
Mchango kutoka kwa Jamii	2,152,981,712
Rekebisho kutokana na kubadilika kwa dhamani ya kubadilisha fedha za kigemi	(2,339,868,805)
Jumla ya Michango	235,655,721,544
Salia anzia 1/7/2011	24,578,395,401
Salio la fedha zilizopelekwa kwa watekelezaji wa Miradi (C)	47,329,118,931
Jumla ya kiasi kilichokuwepo kwa matumizi	307,563,235,875

Kiasi cha fedha kilichochangiwa na washirika wa maendeleo kimeonyeshwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 5: Mchango Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

Wahisani	Kiasi (Sh.)
Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA)	49,169,068,290.00
Shirika la Maendeleo la Kijerumani (KFW)	20,782,467,442.20
Banki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)	79,123,840,658.99
Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID)	15,038,100,000.00
Serikali ya Uholanzi	17,150,886,282.33
JUMLA	181,264,362,673.52

3.1.2 Matumizi ya Fedha za Mradi

Tathmini ya taarifa ya mapato na matumizi ya fedha katika kipindi cha 2011/2012 inaonyesha kuwa, sekta hii ilipokea kiasi cha Sh.307,563,235,875 kutoka serikali ya Tanzania na wadau wengine wa maendeleo, hata hivyo sekta hii iliweza kutumia kiasi cha Sh. 148,926,145,182 na kufanya salio la kufunga mwaka kuwa Sh. 158,637,090,693, kama ulivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 6

Jedwali Na 6: Mapokezi na Matumizi ya Fedha

Na.		Kiasi (Sh.)	Kiasi (Sh.)
	Fedha zilizopatikana		307,563,235,875
	Vifungu vya matumizi		
1	Usimamizi wa	5,674,821,444	

	Rasilimali Maji		
2	Huduma za maji vijijini	33,607,138,606	
3	Huduma za maji taka mijini	100,625,494,220	
4	Kujengea uwezo wa maji (kisekta)	9,018,693,212	148,926,145,182
Salio tarehe 30/6/2012			158,637,090,693

Aidha kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Halmashauri 131 zilipatiwa kiasi cha Sh.88,303,090,628 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji.

Hata hivyo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, Halmashauri zilikuwa na salio la fedha zisizotumika kiasi cha Sh. 64,556,055,033 sawa na 73% ya fedha zilizopokelewa. Salio hili kubwa lilitokana na Halmashauri husika kushindwa kutekeleza miradi iliyokusudiwa. Rejea kiambatisho I

3.2 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

3.2.1 Mapato ya Mfuko

Mfuko wa Maendeleo ya jamii (TASAF) ulianzishwa mwaka wa fedha 2005/2006 na utadumu kwa miaka minne.

Mfuko huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (IDA). Mkataba kati ya Tanzania na Benki ya Dunia ulisainiwa tarehe 19 Januari; 2005 kwa kiasi cha jumla ya Dola za Kimarekani milioni 150. Kiasi cha Sh.Milioni 129 zilitokana na mkopo toka Benki ya Dunia na Dola za Kimarekani milioni 21 zilitokana kama ruzuku.

Jumla ya Sh. 55,701,277,978.52 zilipokelewa na mradi kiasi hiki kilijumuisha bakaa ya Sh. 14,848,919,201.49 ya miaka iliyopita.Hadi kufikia tarehe 30/06/2012 kulikuwa na salio la Sh.12,815,934,118.93 hii ina

maanisha Sh.42,885,345,855.59 zilitumika katika utekelezaji wa miradi. Jedwali Namba 7 linaonyesha hapa chini:

Jedwali Na. 7: Chanzo cha Fedha na Matumizi

	Kiasi (Sh.) 2011/2012	Kiasi (Sh.) 2010/2011
Salio la mwanzo wa mwaka	14,848,919,201.49	23,471,221,514.31
Benki ya Dunia	39,288,285,626.43	52,648,178,990.91
Mchango wa Serikali	0	0
Wengine	1,564,073,150.60	6,981,100,690.04
Mapato kwa mwaka	55,701,277,978.40	83,100,501,195.26
Matumizi kwa mwaka	42,885,343,855.59	68,251,581,997.77
Salio la kufunga mwaka	12,815,934,118.93	14,848,919,201.49

3.2.2 Fedha iliyopelekwa katika Halmashauri

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya Sh. 39,915,181,983 zilipelekwa kwenye Halmashauri, kiasi hiki kilijumuisha bakaa ya Sh. 6,376,697,957 ya miaka iliyopita.

Hadi kufikia tarehe 30/06/2012 kulikuwa na salio la kiasi cha Sh.5,807,528,697 sawa na 14% ya fedha iliyopelekwe katika Halmashauri. Bakaa hii ilitokana na kutokutekelezwa kwa miradi kama ilivyokuwa imepangwa. (Rejea kiambatanisho II)

Jedwali Na. 8:Fedha zilizopelekwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Saliola mwanzo wa mwaka 1/7/2011	6,376,697,957
Fedha iliyopokelewa	33,538,484,026
Jumla	39,915,181,983
Matumizi	34,107,653,286
Salio la kufunga mwaka 30/6/2012	5,807,528,697

Aidha,kiasi cha Sh.39,288,285,626.43 (sawa na Dola za Kimarekani 24,252,028.16) kilitolewa ikiwa ni sehemu ya fedha za ziada kwa mfuko wa kuhudumia jamii awamu ya kwanza na ya pili (kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 30milioni na milioni 35 kwa pamoja) Kiasi hiki kilitolewa kwa ajili ya kuondoa upungufu wa chakula kwa Halmashauri zilizokuwazinakabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula uliotokana na ukame wa muda mrefu.

Mikoa ya Lindi na Mtwara ilipokea Sh.1,564,073,150.60 sawa na Dola za Kimarekani 965,477.26 kutoka Shirika la Mataifa yanayosafirisha Mafuta ya Petrol (OPECII) ikiwa ni awamu ya pili kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali.

3.3.0 Programu ya Maendeleo Katika Sekta ya Kilimo

3.3.1 Utangulizi

Programu hii inajumuisha mipango ya kuendeleza kilimo Kitaifa na kisekta inayofadhiliwa kwa pamoja kupitia mfuko wa washirika wa maendeleo katika sekta ya kilimo.

Programu hii inafuta mpango wa awali wa programu ya maendeleo ya kilimo na mpango wa maendeleo katika Wilaya (DADP).

Tanzania imeridhiampango mkakati (ASDS) ambao umeweka mwongozo wa kufikia malengo.

Mwongozo wa programu ya maendeleo ya kilimo (ASDP) ulianzishwa kwa pamoja na Wizara tano za kisekta ambazo hutoa mwongozo na mchakato wa kutekeleza mpango mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo (ASDS). Shughuli za maendeleo kitaifa zitazingatia mpango mkakati wa Wizara ambapo shughuli za maendeleo katika Wilaya zitatekelezwa na mamlaka za Serikali za mitaa (LGAs).

3.3.2 Mfuko wa Kuchangia Sekta ya Maendeleo ya Kilimo - Hazina

Programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo inapata fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo, mikopo, na michango ya wahisani mbalimbali wakiwemo Ubalozi wa Ireland na Ujapani, Muungano wa Ulaya, Shirika la kimataifa la Maendeleo na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Programu ya Maendeleo ya Kilimo nchini ilipokea Dola za Kimarekani 60,487,612.54 kutoka kwa washirika wa maendeleo na vilevile kulikuwa na salio anzia kiasi cha Dola za kimarekani 12,095,964.03 na kufanya fedha zilizokuwepo kuwa Dola za kimarekani 72,583,576.57. kwa upande mwingine, kiasi ambacho kiliamishwa kutoka accounti ya programu

ya Maendeleo ya Kilimo ni Dola za Kimarekani 57,780,498.22, hivyo kiasi cha fedha kilichobaki mwishoni mwa mwaka ambacho hakukupelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ni jumla ya Dola za Kimarekani 14,803,078.35. Mchanganuo wa michango ya washirika wa maendeleo ni kama ifuatavyo kwenye jedwali namba. 8 hapa chini:

Inasikitisha sana kuona kiasi cha Dola za Marekani 1,011,173.32 ambazo hazikutumiwa na watekelezaji wa miradi pamojana kiasi cha fedha kilichobaki mwishoni mwa mwaka ambacho hakikuhamishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Dola za Kimarekani 14,803,078.35, ambapo imesababisha kutotekelezwa kwa shughuli za miradi kama ilivyokuwa imepangwa.

Jedwali Na. 8: Akaunti kuu ya Mradi

Description	2011/12
Akaunti Na. 9931206251	Kiasi (Dola za Marekeni)
Salio anzia 1/7/2011	12,095,964.03
Shirika la kimataifa la maendeleo- Benki ya Dunia	41,222,776.43
Mkopo kutoka Shirika la kimataifa la maendeleo ya kilimo (IFAD)	18,253,662.79
Kiasi ambacho hakikutumika kwenye miradi	1,011,173.32
Jumla ya fedha	72,583,576.57
Kiasi cha fedha kilichohamishwa	
Wizara ya Kilimo na Ushirika	9,819,975.12
Halmashauri	44,652,645.46
Wizara ya Mifugo na Uvuvi	2,675,834.32
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	184,850.32
Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko	447,193.00
Jumla ya kiasi cha fedha kilichohamishwa	57,780,498.22
Salio ishia 30/6/2012	14,803,078.35

Kuwepo kwa bakaa mwisho wa mwaka 2011/2012 katika wizara ya Fedha inatokana na kazi ambazo hazikukamilika katika kipindi cha mwaka husika.

Fedha zilizohamishwa kwenda kwenye Wizara kama ilivyoonyeshwa hapo juu zilijumuishwa kwenye fungu la maendeleo la Wizara husika na kukaguliwa ipasavyo.

3.3.3 Fedha zilizohamishwa karibia na mwisho wa mwaka wa fedha Dola za Marekani 863,083.78

Pia tuliona kuwa tarehe 25 ya mwezi Juni 2012 siku tano kabla ya mwaka wa fedha kuisha, wizara ya Fedha ilihamisha kiasi cha Dola za Kimarekani 863,080.78 ambazo ni sawa na kiasi cha fedha za Kitanzania Shilingi 1,367,983,036.30 kwenda kwenye taasisi na mawakala wa kutekeleza miradi kupitia barua yenye kumbukumbu namba EB/AG/20/03/VOL.V/70 kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya maendeleo katika sekta ya kilimo.

Hakuna maelezo sahihi yalitolewa kuhusu ucheleweshwaji wa fedha kutumwa kwa watekelezaji wa miradi ya kilimo, ukizingatia kuwa kiasi chote cha fedha kinachobaki mwishoni mwa mwaka kinatakiwa kurudishwa kwenye akaunti kuu ya mradi.

Kwa ujumla kiasi cha fedha ambacho kimehamishwa kwa mwaka wa fedha 2011-2012 ni jumla ya Dola za Kimarekani 57,780,498.22 ambacho kimeshuka kwa asilimia ishirini sawa na Dola za kimarekani 14,375,699.85 ukilinganisha na kiasi cha Dola za Kimarekani 72,156,198.08 ambazo zilihamisha mwaka wa fedha 200/2011. Kiasi kidogo cha fedha ambacho kimetolewa mwaka huu ukilinganisha na mwaka jana kimekwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa imekusudiwa.

Upungufu huu wa fedha una madhara katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli ambazo zilikusudiwa kutekelezwa.

3.3.4 Fedha zilizotumwa kwenda Halmashauri

Katika mwaka wa 2011/2012 halmashauri ilikuwa na jumla ya shilingi 106,781,540,844.89 kiasi hicho kinajumuisha salio anzia la shilingi 27,326,841,575.53 ikiwa ni bakaa ya fedha inayotokana na kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 kwa ajili ya utekelezaji shughuli za programu ya maendeleo katika sekta ya

kilimo. Maelezo ya kina kwa kila halmashauri yako kwenye (kiambatisho III)

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, kulikuwa na bakaa ya shilingi 32,237,919,190.67, hii inaonyesha kuwa halmashauri ziliweza kutumia shilingi 74,543,621,654.22 sawa na asilimia 78.30 ya fedha iliyokuwepo kwa ajili ya kutekeleza shughuli za programu ya maendeleo katika sekta ya kilimo. Mchanganuo ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali namba 10 hapa chini:-

Jedwali Na.10: Vyanzo vya fedha Programu ya Kilimo

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia 1/7/2011	27,326,841,575.53
Kiasi kilichopokelewa	79,454,699,269.36
Jumla ya fedha zilizopo	106,781,540,844.89
Kiasi kilichotumika	74,543,621,654.22
Bakaa hadi 30 Juni, 2012	32,237,919,190.67

3.3.5 Fedha zilizotumwa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Katika mwaka wa 2011/2012 ofisi ya waziri mkuu tawala za mikoa na serikali za mitaa ilikuwa na jumla ya shilingi 300,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu ya kilimo. Hadi kufikia tarehe 30 June 2012 kulikuwa na bakaa ya shilingi 4,329, hii inaonyesha kuwa kutumia shilingi shilingi 299,995,671 zilitumika sawa na asilimia 100% ya fedha zilizokuwepo. Mchanganuo ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na 11 hapa chini:

Jedwali Na 11: Mchanganuo wa fedha za TAMISEMI

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia 1/7/2011	0.00
Kiasi kilichopokelewa	300,000,000.00
Jumla ya fedha zilizopo	300,000,000.00
Kiasi kilichotumika	299,995,671.00
Bakaa hadi 30 Juni, 2012	4,329.00

3.4 Ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya

3.4.1 Utangulizi

Washirika wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya nchini huchangia fedha kupitia akaunti maalumu katika Benki kuu ya Tanzania na baadaye kuhamisha fedha hizo kwenda Wizara ya Afya. TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa fedha kwa mgao wa robo mwaka kupitia Akaunti ya Hazina. Ufadhili huu hufuata mfumo wa Benki kuu ya Tanzania ambapo mihadi ya Washirika wa maendeleo hujumuishwa na kuwa sehemu ya bajeti ya mwaka ya taasisi husika.

Mfuko wa maendeleo ya Afya hauhifadhiwi katika akaunti pekee bali huwekwa pamoja katika akaunti ya maendeleo ya Wizara na Akaunti na.6 ya katika Halmashauri, inayotumika pia kutokana na vyanzo vingine

3.4.2 Uchambuzi wa Fedha Mfuko wa Maendeleo ya Afya

Mfuko wa maendeleo ya Afya hupata michango ya fedha kutoka kwa mashirika ya Maendeleo. Mfuko huu ulipokea katika mwaka huu wa fedha kiasi cha Dola za Marekani 104,121,619.02 kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini na dola za marekani 386,033.17 zilirejeshwa na wizara ya afya na ustawi wa jamii. Kulikuwa na salio la kuanzia la dola zakimarekani 3,806,363.71 na hivyo kufanya kiasi kilichokuwepo kuwa dola za kimarekani 108,314,015.9. Fedha za mradi huu huwekwa katika akaunti za kigeni kwa mfumo wa dola za kimarekani katika akaunti iliyopo benki kuu ya Tanzania chini ya usimamizi wa mhasibu mkuu wa serikali kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba 12 hapa chini:

Jedwali la 12 Vyanzo vya Fedha vya Mfuko wa Maendeleo ya Afya

Mashirika Ya Maendeleo	Kiasi (Dola za Marekani)
UNDP	600,000.00
Ubalozi wa Denmak	17,942,000.00
Ireland	8,810,100.00

Uholanzi	20,694,669.62
CIDA	24,492,995.00
KFW	9,430,169.00
Uswisi	3,244,997.30
Uholanzi	2,690,204.01
Mfuko wa Umoja wa Mataifa Maendeleo ya Watoto	1,000,000.00
Norway	5,216,484.09
IDA	10,000,000.00
Jumla Ndogo ku	104,121,619.02
Salio la mwaka 2010/2011	386,033.17
Salio la Kuanzia Mwaka 01 July 2011	3,806,363.71
Jumla Kuu	108,314,015.9

3.4.3 Uhamishaji wa fedha kwenda kwa Wadau wa Maendeleo kiasi cha dola za kimarekani 106,152,921.27

Katika mwaka unaofanyiwa ukaguzi kiasi cha dola za marekani 106,162,678.27 kiliamishwa kwenda kwa wadau wa maendeleo na kufanya salio la kufungia mwaka kuwa dola za kimarekani 2,161,094.9 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012 kama inavyoonyeshwa katika Jedwali namba 13 hapo chini:

Jedwali 13: Mapokezi na Uhamishaji wa fedha kwenda kwa Wadau

Mapokezi ya fedha	Kiasi (Dola za Kimarekani)
Kiasi Kisichotumika Mwaka 2010/2011	386,033.17
Salio la Kuanzia 01 Julai 2011	3,806,363.71
UNDP	600,000.00
Ubalozi wa Denmark	17,942,000.00
Ireland	8,810,100.00
Uholanzi	23,384,873.63
CIDA	24,492,995.00

KFW	9,430,169.00
Uswisi	3,244,997.30
UNICEF	1,000,000.00
Norway	5,216,484.09
IDA	10,000,000.00
Jumla Mapokezi ya fedha	108,314,016.17
UHAMISHAJI	
Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	52,414,115.83
Serikali za Mitaa	53,297,699.56
TAMISEMI	441,105.86
Jumla ya Fedha Zilizohamishwa	106,152,921.27
Salio linaloishia 30/6/2012	2,610,949.6

3.4.4 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Vyanzo vya Fedha

Wahisani wa maendeleo huchangia fedha zao katika mfuko wa pamoja kwenye akaunti kuu iliyopo benki kuu ya Tanzania na baadae fedha hizo hupelekwa wizara ya afya na ustawi wa jamii kwa mfumo wa obo mwaka. Uchangiaji kwenye wizara hupitia mfumo wa kawaida wa usimamizi wa Fedha benki kuu ambapo mihadi ya kifedha hujumuishwa katika bajeti ya mwaka wa wizara.

Fedha kutoka katika mfuko wa kuchangia hupelekwa katika Wizara ya Afya na ustawi wa jamii na hutolewa katika mfumo wa kawaida wa serikali wa kugawa fedha. Fedha za mfuko za uchangiaji huwa sehemu ya fedha zinazotunzwa Benki kuu na kutolewa kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii kwa matumizi yake. Sambamba na hilo fedha za mfuko maendeleo ya afya zinazotunzwa katika akaunti tofauti bali huchanganywa katika akaunti ya maendeleo ambayo huchangiwa pia na vyanzo vingine vya maendeleo.

Katika mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2012 wizara ilipokea shilingi 71,043,000,000. Matimizi halisi 70,081,984,500 na kufanya salio la fedha zisizotumika

kuwa shilingi 1,024,015, 500 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012 ambapo shilingi 700,000,000 zilihamishwa kwenda akaunti ya amana ma shilingi 324,015,500 zilihamishiwa akaunti kuu iliyoko benki kuu ya Tanzania kama inavyoonyeshwa katika Jedwali namba 14 hapo chini:-

Jedwali 14: Vyanzo vya Fedha kwa Mfuko wa Maendeleo ya Afya - Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Maelezo	Kiasi (Shilingi)
Mapokezi	71,043,000,000
Matumizi	70,081,984,500
Salio	1,024,015, 500
Uhamisho kwenda Akaunti ya Amana	700,000,000
Uhamisho kwenda Akaunti Kuu	324,015,500

3.4.5 TAMISEMI

Programu ya Sekta ya Afya huchangiwa na Ireland, Uholanzi, Norway, Ujerumani na Benki ya Dunia, Shirika la Uswisi la Maendeleo na Ushirikiano katika mwaka 2011/2012 ilipokea kiasi cha shilingi 687,000,000.00.

Kwa mujibu wa taarifa ya mapato na matumizi TAMISEMI ilikuwa na kiasi cha fedha kwa ajili ya program hii cha shilingi 913,514,758.02 kuhusisha salio la kuanzia la shilingi 226,514,758.02. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 kulikuwa nakiasi kisichotumika shilingi 512,637,403.42 sawa na asilimia 56 kuashiria kwamba mradi ulitumia shilingi 400,877,354.60 sawa na asilimia 44 kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba 15 hapo chini:-

Jedwali 15: Vyanzo vya fedha kwa mfuko wa Maendeleo ya Afya TAMISEMI

Maelezo	Kiasi (Sh.)
	226,514,758.02
Fedha za Kuanzia	
Ongeza: Mapokezi ya Fedha	687,000,000,00
Kiasi kilichopatikana	913,514,758.02
Toa: Matumizi	400,877,354.60
Kiasi kilichosalia mpaka tarehe 30/06/2012	512,637,403.42

3.4.6 Serikali za Mitaa

Katika mwaka wa fedha serikali za mitaa zilipokea fedha kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba 16 na kuonyesha kwa undani katika kiambatisho namba IV.

Jedwali namba 16: Vyanzo vya Fedha Mfuko wa Maendeleo 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Shilingi)
Salio la Kuanzia tarehe 1/7/2011	8,782,526,242
Ongeza: Fedha zilizopokelewa	80,435,231,856
Kiasi Kilichopatikana	88,805,785,681
Toa: Matumizi	76,812,025,208
Kiasi kilichobakia tarehe 30/6/2012	12,313,520,449

3.5 Miradi Mingine

3.5.1 Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria

3.5.1.1 Taarifa ya fedha - Hazina

Katika mwaka wa fedha 2011/12 Wizara ya Fedha ilipokea kiasi cha Dola za Kimarekani 102,798,691 ikiwa sawa na Sh. 161,933,708,651.28 kutoka katika mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Kifua kikuu, Ukimwi na Malaria. Kati ya fedha hizo kiasi cha Sh.

155,925,146,179.06 ziliwekwa katika akaunti na 9931206811 (Mfuko wa Kimataifa wa kupambana na Ukimwi na Kifua Kikuu na Malaria (mzunguko wa Nane) unaotunzwa Benki Kuu ya Tanzania. kiasi cha Sh. 5,438,151,897.33 kilikwenda Tume ya UKIMWI na kiasi cha Sh. 570,410,574.89 kilikwenda Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kama inavyoonekana hapa chini kwenye jedwali namba 17:

Jedwali 17:Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Kiasi toka mfuko wa kimataifa kwenda Wizara ya fedha	161,933,708,651.28
Uhamisho wa fedha kwenda:	
Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii	155,925,146,179.06
Tume ya kudhibiti UKIMWI	5,438,151,897.33
Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	570,410,574.89

3.5.1.2 Programu ya Kudhibiti Malaria-(ACT)

3.5.1.2 Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Malaria

Programu ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI ilipewa Sh 32,162,839,278. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh.63,175,979 kilikuwa ni salio la fedha la mwaka uliopita. Hadi kufikia tarehe 30/6/2012 matumizi yalikuwa Sh.29,344,141,578 ikiwa ni sawa na asilimia 91 ya fedha yote iliyokuwepo; hivyo kufanya salio ishia kuwa Sh. 2,818,698,100,kama inavyoonekana kwenye jedwali Namba. 18 hapa chini:

Jedwali Na.18: Mapato na Matumizi

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia	63,175,979
Fedha iliyopokelewa	32,099,663,699
Fedha iliyopo kwa ajili ya matumizi	32,162,839,278
Matumizi	29,344,141,578
Salio ishia	2,818,698,100

3.5.1.3 Kitengo cha Uchunguzi wa Magonjwa

Kitengo cha Uchunguzi wa magonjwa kilikuwa na kiasi cha Sh 3,047,885,860. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh.2, 939,824,392 kilikuwa ni salio la fedha la mwaka uliopita. Hadi kufikia tarehe 30/6/2012 matumizi yalikuwa Sh.1,451,479,842 ikiwa ni sawa na asilimia 48 ya fedha yote iliyokuwepo; hivyo kufanya salio ishia kuwa Sh.1,596,406,018 kama inayoonekana kwenye jedwali Namba. 19 hapa chini:

Jedwali 19: Mapato na matumizi Kwa mwaka wa fedha 2011/2012-Kitengo cha Uchunguzi wa Magonjwa

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia	2, 939,824,392
Fedha iliyopokelewa	108,061,468
Jumla ya Fedha iliyopo	3,047,885,860
Matumizi	1,451,479,842
Salio ishia	1,596,406,018

3.5.1.4 Programu ya Kupambana na Kifua Kikuu na Ukoma - Mzunguko wa Sita

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 programu ya kitaifa ya kupambana na kifua kikuu na ukoma ilikuwa na kiasi cha Sh. 9,549,945,620 ambapo kiasi cha Sh.3, 504,768,943 kilikuwa ni salio la kipindi kilichopita ikijumuisha na hundi zisizowasilishwa benki za kiasi cha Sh.340,815,604.

Wakati huohuo, matumizi halisi ni Sh. 7,848,648,422.70 ikiwa ni asilimia 83 ya fedha yote na kuwa na bakaa ya mwaka ya kiasi cha Sh. 1,360,481,593 kama inavyoonekana katika jedwali namba 20 hapa chini.

Jedwali 20: Mapato na Matumizi Mzunguko wa Sita kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Melezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia	3, 504,768,943
Kiasi kilichopokelewa	6,045,176,677
Hundi zilizochacha	340,815,604
Kiasi cha fedha kilichopo	9,549,945,620
Matumizi	7,848,648,423
Salio ishia	1,360,481,593

3.5.1.5 Mfuko wa Kimataifa wa kupambana na Malaria Mzungukowa nane -Programu ya kitaifa ya kusaidia vyandarua

Katika kipindi mwaka 2011/2012 Programu ya Kitaifa ya Kusaidia Vyandarua ilikuwa na kiasi cha Dola za Kimarekani 24,632,497 ambapo kiasi cha Dola za Kimarekani 20,704,329 kilikuwa ni salio la kipindi kilichopita

Wakati huohuo, matumizi halisi ni Dola za Kimarekani.23,567,117 ikiwa ni asilimia 96 ya fedha yote na kuwa na bakaa ya mwaka ya kiasi cha Dola za Kimarekani 1,065,380 kama inavyooneka katika jedwali namba 21 hapa chini.

Jedwali 21:Mapato na Matumizi Mzungukowa nane - Programu ya kitaifa ya kusaidia vyandarua kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Dola za Kimarekani)
Salio anzia	20,704,329
Kiasi kilichopokelewa	3,928,168
Jumla ya Fedha iliyopo	24,632,497
Matumizi	23,567,117
Salio linaloishia	1,065,380

3.5.1.6 Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti UKIMWI

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti UKIMWI ilikuwa na kiasi cha Sh.6,038,729,954 ambapo kiasi cha Sh.4,427,030,560 kilikuwa ni salio la kipindi kilichopita.

Wakati huohuo, matumizi halisi ni Sh. 4,106,585,003 ikiwa ni asilimia 68 ya fedha yote na kuwa na bakaa ya mwaka ya kiasi cha Sh.1,932,144,951 kama inavyooneka katika jedwali namba 22 hapo chini:

Jedwali 22: Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Sh.)2011/2012
Salio anzia	4,427,030,560
Kiasi cha Fedha iliyopokelewa	1,611,699,394
Kiasi cha Fedha yote iliyopo	6,038,729,954
Matumizi	4,106,585,003
Salio linaloishia	1,932,144,951

3.5.1.7 Ufuatiliaji na tathimini ya Mfuko wa Kimataifa mzunguko wa nane-Wizara ya Afya na Ustawi Wa Jamii

Katika kipindi mwaka 2011/2012 Ufuatiliaji na tathimini Mfuko wa Kimataifa ilikuwa na kiasi cha Sh.102,569,551 ambapo kiasi cha Sh.44,826,851.14 kilikuwa ni salio la kipindi kilichopita.

Wakati huohuo, matumizi halisi ni Sh.43,795,150.00 ikiwa ni asilimia 43 ya fedha yote na kuwa na bakaa ya mwaka ya kiasi cha Sh.58,774,401.14 kama inavyoonyesha katika jedwali namba 23 hapo chini.

Jedwali 23:Mapato na Matumizi mzunguko wa nane kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia	44,826,851.14
Kiasi cha fedha kilichopokelewa	57,742,700.00
Kiasi cha fedha iliyopo	102,569,551.14
Matumizi	43,795,150.00
Salio ishia	58,774,401.14

3.5.1.8 Mfuko wa Kimataifa Mzunguko wa nane Akaunti fedha za kigeni Benki kuu

Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa na kiasi cha dola za Kimarekani 94,330,124 kutoka kwenye Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria na UKIMWI kiasi kilichotumika ni dola za Kimarekani 81,565,837sawa na asilimia 86 ya kiasi kilichotolewa hivyo, kubaki na salio la dola za Kimarekani12,764,287 kama inavyonekana hapa chini kwenye jedwali 24;

Jedwali 24: Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia	27,156,536
Kiasi kilichopokelewa	67,173,588
Kiasi cha fedha iliyopo	94,330,124
Matumizi	81,565,837
Salio ishia	12,764,287

3.5.1.9 Bohari Kuu ya Madawa

Bohari Kuu ya Madawa ilikuwa na kiasi cha Sh.99,996,669,157kutoka kwenye Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria na UKIMWI. Kiasi kilichotumika cha Shs. 56,878,585,838 ni sawa na asilimia 60 ya kiasi kilichotolewa hivyo, kubaki na salio la Sh. 31,920,182,964 kama inavyoonekana hapa chini kwenye jedwali 25;

Jedwali 25: Mapato na Matumizi Bohari Kuu ya Madawa kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia	4,788,172,713
Kiasi kilichopokelewa	95,208,496,444
Kiasi cha Fedha iliyopo	99,996,669,157
Matumizi	59,878,585,838
Salio ishia	40,118,083,319

3.5.1.10 Uimarishaji Mfumo wa Afya-Mfuko wa Kimataifa mzunguko wa Tisa (9)

Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii ilikuwa na kiasi cha Sh. Sh.7,365,984,396.30 kutoka kwenye mfuko wa kimataifa wa kupambana na malaria na UKIMWI katika uimarishaji wa Mfumo wa Afya mzunguko wa tisa. Kiasi kilichotumika ni Sh. 4,578,057,698.80sawa na asilimia 62 ya kiasi kilichotolewa hivyo, kubaki na salio la Sh. 2,787,926,698 kama inavyoonekana hapa chini kwenye jedwali 26.

Jedwali 26: Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Salio anzia	475,800,119.60
Kiasi kilichopokelewa	6,890,184,276.70
Kiasi cha fedha kilichopo	7,365,984,396.30
Matumizi	4,578,057,698.80
Salio ishia	2,787,926,697.50

3.5.1.11 Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikuwa na kiasi cha Sh.400,432,750 kutoka kwenye Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria na UKIMWI Kiasi kilichotumika ni Sh. 324,637,410 sawa na asilimia 81 ya kiasi kilichotolewa hivyo, kubaki na salio la Sh. 75,795,340kama inavyoonekana hapa chini kwenye jedwali 27;

Jedwali 27: Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha -2011/2012

Maelezo	kiasi (Sh.)
Salio anzia	63,944,387
Kiasi kilichopokelewa kwa mwaka	90,410,575
Kiasi kilicholipwa na wadaiwa	246,077,788
Kiasi cha fedha iliyopo	400,432,750
Matumizi	324,637,410
Salio ishia	75,795,340

3.5.1.12 Global Fund (GF) - TACAIDS Funds

Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania ilikuwa na kiasi cha Sh.6,193,977,084 kutoka kwenye Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria na UKIMWI Kiasi kilichotumika niSh. 4,774,161,160 ni sawa na asilimia 77 ya kiasi kilichotolewa hivyo, kubaki na salio la Sh. 1,419,815,924 kama inavyonekana hapa chini kwenye jedwali 28;

Jedwali 28: Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012

Maelezo	Kiasi (Ss.)
Salio anzia	932,643,027
Kiasi kilichopokelewa	5,261,334,057
Fedha yote iliyopo	6,193,977,084
Matumizi	4,774,161,160
Salio ishia	1,419,815,924

3.5.2 Miradi Mingine ukiondoa Mfuko wa Kimataifa wa kupambana na UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu na Ukoma

Taarifa ya utendaji wa fedha kwa miradi mingine ambayo ilitathiminiwa ilifikia 93. Masuala muhimu yaliyozingatwa ni salio anzia, kiasi kilichopokelewa, matumizi kwa mwaka na salio ishia mwisho wa mwaka. Angalia mchanganuo katika **kiambatisho V**

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UKAGUZI

4.0 Utangulizi

Sura hii inatoa uchambuzi wa masuala yaliyosababisha kutoa hati aina fulani kwa mkaguliwa. Uchambuzi unalenga kuelezea

misingi iliyotumika kufikia maamuzi ya kutoa aina moja au nyingine ya hati za ukaguzi.

Katika mwaka wa fedha 2010/2011, miradi minne mikubwa inayofadhiliwa na wahisanina miradi mingine midogo hamsini na nne (54) ilikaguliwa na kufanya jumla ya miradi iliyokaguliwa kufikia hamsini na nane (58).

4.1 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

4.1.1 Utangulizi

Awamu ya pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ilianzishwa baada ya kusainiwa kwa makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Tanzania na Benki ya Dunia kupitia Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo (IDA). Makubaliano hayo yalisainiwa tarehe 19 Januari, 2005 na kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii awamu ya pili (TASAF II) ambao unashirikishwa katika Mkakati wa Taifa wa Kuinua Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) ulioanzishwa kwa madhumuni ya kuiwezesha jamii kupata nafasi za kuchangia na kuimarisha maisha ikihusishwa na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG).

Kwa mujibu wa hadidi za rejea zilizomo kwenye mwongozo wa utendaji wa TASAF, madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kumwezesha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maoni yake kuhusu taarifa za fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

4.1.1.2 Malengo ya Mradi

Awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii (TASAF II) ilianzishwa kuwezesha jamii kupata fursa ya kuchangia kuboresha maisha ili kufikia malengo ya milenia katika mkakati wa kupunguza umaskini. TASAF II pia inalenga:

- (i) Kusaidia uundwaji wa vikundi vya hiari vya kuweka fedha
- (ii) Kutoa huduma kwa jamii ambayo itachangia upatikanaji wa huduma za msingi na hifadhi ya mazingira unaofuata Mpango wa Maendeleo ya Milenia.
- (iii) Kutoa nafasi za ajira kwa wasiojiweza, chakula kwa maskini na kuongeza kipato chao, ujuzi na nafasi za kazi kwa maafisa fedha wa vijiji.
- (iv) Kutoa msaada kwa yatima, wasiojiweza, wazee na walioathirika na virusi vya ukimwi waweze kujimudu kiuchumi.

4.1.1.3 Usimamizi wa Miradi

(i) Kitaifa

Awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii (TASAF II) katika ngazi ya Taifa unasimamiwa na kitengo cha Usimamizi cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TMU) kinachoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji. Kitengo hiki huratibu na kutekeleza shughuli za kila siku za awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii (TASAF II). Mkurugenzi Mtendaji huwajibika kwa Kamati ya Uongozi (NSC) kwa maswala yote ya utawala na fedha yanayohusu shughuli za awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii.

(ii) Ngazi ya Halmashauri

Katika ngazi ya Wilaya, Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DED)/ Wakurugenzi watendaji wa Manispaa (MD) wakiwa ni watendaji wa Wilaya/Manispaa kwa uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, husaidia uendeshaji wa awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii kwa kuwaongoza Waratibu wa fedha wa vijiji (VFC). Waratibu wa fedha wa vijiji (VFC) huteuliwa na Baraza la Wilaya kutoka miongoni mwa watu wenye sifa katika Halmashauri/Manispaa kwa mujibu wa hadidi za rejea zitolewazo na Kitengo cha Uongozi cha TASAF (TMU). Waratibu wa fedha wa vijiji (VFC) huratibu shughuli za awamu ya pili ya Mfuko wa

Jamii (TASAF II) katika ngazi ya wilaya kwa kuhamasisha na kuwezesha jamii katika maswala yanayohusu utekelezaji wa miradi midogo ya jamii. Mratibu wa fedha wa Kijiji (VFC) anawajibika kwa Kitengo cha Uongozi cha TASAF (TMU) kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

Ifuatayo ni orodha ya Halmashauri zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2011/2012, aina ya hati za ukaguzi zilizotolewa pamoja na sababu za kutolewa kwa hati hizo.

(a) Jedwali Na. 29: Hati inayoridhisha bila maswala ya msisitizo

Kati ya Halmashauri 127 zilizokaguliwa ni Halmashauri ishirini na nane (28) sawa na asilimia ishirini na mbili (22%) zilipata hati inayoridhisha kama zilivyoorodheshwa hapa chini:

Na	Halmashauri
1	Bukombe
2	Mji mdogo wa Korogwe
3	Manispaa ya Moshi
4	Mwanga
5	Jiji la Tanga
6	Manispaa ya Lindi
7	Nachingwea
8	Lindi
9	Mkuranga
10	Mji mdogo wa Kibaha
11	Manispaa ya Bukoba
12	Iramba
13	Kibondo
14	Manispaa ya Temeke
15	Manispaa ya Mtwara
16	Newala
17	Mtwara

18	Njombe
19	Mvomero
20	Ukerewe
21	Kilosa
22	Manispaa ya Ilala
23	Ulanga
24	Singida
25	Maniapaa ya Singida
26	Tunduru
27	Mbozi
28	Manispaa ya Morogoro

(b) Jedwali Na. 30: Halmashaurizilizopata hati zinazoridhisha pamoja na masuala ya msisitizo

Kati ya Halmashauri 127 zilizokaguliwa Halmashauri sabini na tano (75) sawa na asilimia hamsini na tisa (59%) zilipata hati zinazoridhisha pamoja na masuala ya msisitizo kama zilizoorodheshwa hapo chini:-

1	Halmashauri ya wilaya ya Bunda
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo ya Sh.3,917,500 hayakuambatanishwa na ripoti ya utekelezaji. • Nyumba iliyoko katika Shule ya sekondari ya Bulamba yenye thamani ya Sh.29,000,600 ilijengwa chini ya kiwango. • Ujenzi wa barabara ya Busamba-Namalama yenye thamani ya Shs.31,920,000 haujakamilika. • Ujenzi wa jengo la Utawala la Kwiramba sekondri lenye thamani ya Sh.40,237,700 haujakamilika.
2	Halmashauri ya wilaya ya Musoma
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri haikutekeleza mapendekezo yote yaliyotolewa na wakaguzi kwa mwaka unaoishia Juni 2011. • Miradi yenye thamani ya Sh. 523,844,347.68 haikukamilika. • Miradi yenye thamani ya Sh.174,123,880 haikutekelezwa.
3	Halmashauri ya Musoma
	<ul style="list-style-type: none"> • Choo cha Shule ya msingi Kigera kilijengwa na kukamilika lakini hakitumiki. Gharama ya ujenzi ni Sh.9,900,000. • Ujenzi wa choo chenye thamani ya Sh.7,937,227.70 shule ya Sekondari ya

	<p>Mwisenge haujakamilika.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa madarasa,choo na jengo la utawala shule ya sekondari Baruti yenye thamani ya Sh.17, 752,394.70 haujakamilika.
4	Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti
	<ul style="list-style-type: none"> • Mchanganuo wa gharama za kazi za ujenzi(BOQ) na mkataba kwa ajili ya ukarabati wa zahanati ya Gesarya haukuwasilishwa wenye thamani ya Sh.12,536,900
5	Halmashuri ya wilaya ya Tarime
	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa jengo la utawala shule ya sekondari ya Masanga lenye thamani ya Sh. 19,453,000 haujakamilika. • Miradi yenye thamani ya Sh.133,382,114.25 haijakamilika.
6	Halmashauri ya wilaya ya Chato
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri haijatekeleza mapendekezo ya wakaguzikwa mwaka unaoishia Juni 2011 kiasi cha Sh. 178,837,976.53 • Utekelezaji wa mradi wenye thamani ya Sh. 11,149,166.00 katika shule ya msingi Kanyindo ulikuwa chini ya kiwango
7	Halmashauri ya wilaya ya Kahama
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh.106,872,585.66 kiliongezwa kimakosa kwenye Mali za kudumu (mitambo, mali na vifaa). -Makosa hayo yalitokana na mali za asili (biological and agricultural assets) na gharama za usimamizi wa shughuli za miradi kuingizwa kwenye mali za kudumu. Hii ni kinyume na mwongozo wa viwango vya Kihisibu vya Kimataifa katika Sekta ya Umma (IPSAS 17 (6)(a) na • Shughuli zenye thamani ya Sh.401,317,010.99 zilizofanyika kwa ajili ya kupunguza uhaba mkubwa wa chakula uliotokana na ukame nyaraka zake hazikuwasilishwa.
8	Halmashuri YA wilaya ya Shinyanga
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri haikutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na wakaguzi kwa mwaka unaoishia Juni 2011 -Shs.105,644,027 • Bwawa la Nyashimbi halitumiki kwa sababu ya ukosefu wa maji unaosababishwa na ukame hali hii imepelekea jamii kutopata huduma iliyotegemea.
9	Halmashauri ya wilaya ya Bariadi
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri ilifanikiwa kutekeleza miradi yenye thamani ya Sh.56,149,714 hata hivyo ilishindwa kuwasilisha ripoti za utekelezaji kama uthibitisho kwa mamlaka husika. • Vijiji vya Nkololo na Mahembe havijakamilisha Ujenzi wenye thamani ya Sh.461,254,234 kwahiyo jamii husika haijafaidika na huduma iliyotarajiwa.
10	Halmashauri ya wilaya ya Kishapu

	<ul style="list-style-type: none"> • Hati za malipo zenye thamani ya Sh.1,650,000 hazikuwasilishwa. • Uchambuzi wa taarifa ya mlingano kati ya bajeti na na kiasi kilichotumika umebaini Sh.888,840 zilitumika zaidi ya zilizokuwa zimeidhinishwa. • Wakati wa uhakiki na mapitio ya utendaji wa miradi ilibainika kuwa miradi yenye thamani ya Sh.181,240,370 ilikuwa haijakamilika. • Taarifa ya usuluhisho wa benki ya 30/6/2012 ilionyesha kuna hundi zenye thamani ya Sh.1,350,000 hazijawasilishwa benki.
11	Halmashauri ya wilaya ya Maswa
	<ul style="list-style-type: none"> • Kulikuwa na bakaa ya Sh.297,035,489 hii inamaanisha kuwa miradi ya thamani hiyo haijakamilika au haijatekelezwa. • Miradi mitano (5) yenye thamani ya Sh.113,274,450 inaendelea kutekelezwa ingawa muda wa kukamilisha miradi hiyo umeishapita na hakuna nyaraka zinazoonyesha kuwa halmashauri ilimuongezea mkandarasi muda wa kukamilisha miradi hiyo. • Ujenzi wa majengo ya idara ya wangonjwa wa nje (OPD) katika zahanati za Mwadila, Kadaganda na Bugarama yenye thamani Shs. 67,337,450.00 umekamilika lakini majengo hayatumiki.
12	Halmashauri ya wilaya ya Meatu
	<ul style="list-style-type: none"> • Kulikuwa na kiasi cha Sh.280,017,479.96 kama salio ishia katika mwaka wa fedha 2011/2012 hii inamaanisha kuwa miradi yenye thamani iliyotajwa haijakamilika au haijatekelezwa. • Kutokana na kukosekana kwa Stakabadhi ya kukiri kupokea fedha kiasi cha Sh.86, 770,387.71 wakaguzi walishindwa kuthibitisha iwapo fedha zilipokelewa na walengwa.
13	Jiji la Mwanza
	<ul style="list-style-type: none"> • Miradi ambayo haikutekelezwa Sh.42,613,450: <ul style="list-style-type: none"> ➤ Ujenzi wa madarasa matatu Mkuyuni shule ya msingi Sh. 25,781,800 ➤ Ujenzi wa nyumba ya mwalimu Kabangaja Sh. 16,831,650 • Utekelezaji wa miradi kumi (10) yenye thamani ya Sh.263,462,686 ulikuwa bado unaendelea hii inamaanisha ucheleweshwaji wa huduma katika jamii husika.
14	Halmashari ya wilaya ya Misungwi
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh. 125,293,524.70 kilionyeshwa kama fedha ambayo haikutumika kwa mwaka, hii inamaanisha kwamba baadhi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2011/12 haikutekelezwa. • Ujenzi wa bwawa lenye thamani ya Sh. 86,852,898.16 haujakamilika.

	<ul style="list-style-type: none"> • Mashine tatu za kusaga zenye thamani ya Sh. 27,681,818.19. Hazijafungwa. • Vijiji vitatu vilipelekewa Shs.39,831,565.45 kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa, ujenzi haujaanza. • Uwezekano wa miradi mitatu ya uvuvi ya vijiji vya Nyamatala,Mwakalima na Mwaniko iliyogharimu Sh.23,473,900 kuwa endelevu ni wa mashaka. • Fedha kwa ajili ya shughuli za utendajizilipokelewa na halmashauri lakini hazikuhamishiwa kwenye miradi husika-Sh.71,235,340. • Sh.2,224,298.00 zililipwa mwaka wa fedha 2011/12 kwa wazabuni mbalimbali ikiwa ni madai ya miaka iliyopita, madeni haya hayakuonyeshwa kwenye Taarifa ya Hesabu hii ni Kinyume na Agizo na.22(1) ya Memoranda ya fedha Mamlaka za Serikali za Mitaa,2009.
15	Halmashauri ya wilaya ya Arusha
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo yenye thamani ya Sh.4,285,000 yalifanyika kwa fedha taslimu hii ni kinyume na Agizo na.22(1) la Memoranda ya fedha Mamlaka za Serikali za Mitaa,2009 • Daftari kwa ajili ya kudhibiti matumizi ya vifungu(vote book) haikuandaliwa kinyume na Agizo na.23(1) na (2) la Memoranda ya fedha Mamlaka za Serikali za Mitaa,2009.
16	Mji mdogo wa Babati
	<ul style="list-style-type: none"> • Kulikuwa na bakaa ya Sh. 77,445,124, hii inamaanisha kwamba baadhi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2011/12 haikutekelezwa.
17	Halmashauri ya wilaya ya Karatu
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri haikuandaa Mpango kazi kwa ajili ya mwaka 2011/2012.Ilikuwa vigumu kwa wakaguzi kutambua kazi zilizotakiwa kufanyika katika mwaka husika.
18	Halmashauri wilaya ya Lushoto
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh. 112,545,105 ilionyeshwa kama fedha ambayo haikutumika kwa mwaka.Hii ilitokana na ucheleweshwaji wa uhamishaji wa fedha katika miradi husika kwa hiyo miradi ya kiasi hicho haikutekelezwa.
19	Halmashauri ya wilaya ya Babati
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh. 31,691,389 ilionyeshwa kama fedha ambayo haikutumika kwa mwaka.Hii inamaanisha miradi yenye thamani hiyo haikutekelezwa.
20	Halmashauri ya wilaya ya Hai
	<ul style="list-style-type: none"> • Sh. 9,792,881.82 zilitolewa kwa ajili ya kilimo cha mbogamboga

	<p>badala yake kilichimbwa kisima kitakacho tumika kwa ajili ya umwagiliaji, mradi uko hatua za mwanzo.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mradi wa mbuzi wa maziwa kijiji cha Tindigani wenye thamani ya Sh.10,349,500 haujakamilika. • Mradi wa kilimo cha vituguu kilichopo katika kijiji cha Mungushi haujakamilika- Sh.8,816,272.73.
21	Halmashauri ya wilaya ya Handeni
	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa bwawa la mradi ulifanyika karibu na bwawa lililojengwa na DADPS. Mabwawa haya yanatumia mkondo mmoja wa maji, hii inapelekea wakati wa mvua maji kutiririkia kwenye bwawa la DADPs na kusababisha bwawa la TASAF kukosa maji. • Utekelezaji usioridhisha wa mradi wa ufugaji wa mbuzi wa maziwa katika vijiji vya Kidereko na Kweisasu wenye thamani ya Sh.21,775,238.
22	Halmashauri ya wilaya ya Kilindi
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh. 139,841,929 ilionyeshwa kama fedha ambayo haikutumika kwa mwaka.Hii inamaanisha miradi yenye thamani iliyotajwa haikutekelezwa. • Taarifa ya fedha ilionyesha fedha iliyotolewa kwa ajili ya mfuko wa vijiji (NVF) tu na haikutoa taarifa ya Sh.34,323,003 ambazo ni fedha za usimamizi wa miradi(operational fund).
23	Halmashauri ya wilaya ya Longido
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh. 356,892,004 ilionyeshwa kama fedha ambayo haikutumika kwa mwaka 2011/12.Hii inamaanisha miradi yenye thamani iliyotajwa haikutekelezwa.
24	Halmashauri ya wilaya ya Meru
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo ya Sh.3,060,000hayakugongwa muhuri wa kuhakiki malipo kabla ya kulipa. • Ucheleweshaji wa ukarabati wa mfumo wa maji katika Kata ya Poli Sh. 27,668,526.30 • Kiasi cha Sh.27,226,436.20ilionyeshwa kama fedha ambayohaikutumika kwa mwaka 2011/12.Hii inamaanisha miradi yenye thamani iliyotajwa haikutekelezwa.
25	Halmashauri ya wilaya ya Mkinga
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh. 19,294,813 ilionyeshwa kama fedha ya miradi ambayo haikutekelezwa.
26	Halmashauri ya wilaya ya Moshi
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh.88,787,895 ilionyeshwa kama fedha ya miradi ambayo

	haikutekelezwa.
28	Halmashauri ya wilaya ya Siha
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh.20,139,333.29 ilionyeshwa kama fedha ya miradi ambayo haikutekelezwa.
28	Halmashauri ya wilaya ya Pangani
	<ul style="list-style-type: none"> • Taarifa za utendaji wa kazi haijawsilishwa. • Sh.236,953,630 zililipwa kwa watu binafsi badala ya kulipiwa kwenye akaunti ya vikundi vya jamii. • Shughuli za miradi zenye thamani ya Sh.4,272,245.83 hazikutekelezwa.
29	Halmashauri ya wilaya ya Morogoro
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri ilipanga kutekeleza miradi ishirini(20)yenye thamani ya Sh.159,878,048.Hata hivyo kutokana na kutokupewa fedha mpaka tarehe 30/6/2012 miradi yote ilikuwa haijatekelezwa. • Halmashauri ilipanga kutekeleza miradi yenye thamani ya Sh.215,877,237 hata hivyo mpaka mwishoni mwa mwaka wa fedha 2011/2012 ni miradi yenye thamani ya Sh.87,055,819 tu ndiyo iliyokuwa imetekelezwa na kuacha miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. 128,821,419 bado haijakamilika.
30	Halmashauri wilaya ya Kilombero
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri ilibadilisha mradi wa ujenzi wa barabara ya Mikumi-Mikolelo na kuwa ujenzi wa daraja bila kibali baada ya kupokea Sh. 33,000,000 badala ya Sh.13,636,363. • Mapungufu yaliyojitokeza ripoti za robo mwaka: <ul style="list-style-type: none"> ➢ Taarifa za maendeleo ya miradi na hali halisi ya utekelezaji wa miradi haziendi sambamba na Taarifa ya fedha. ➢ Taarifa za maendeleo hazikuonyesha hatua/hadhi ya utekelezaji wa baadhi za miradi ulipofikia. ➢ Ripoti za robo mwaka hazikuonyesha bajeti iliyopitishwa, fedha ambazo hazikutolewa, kiasi ilichotumika na bakaa.
31	Halmashauri ya wilaya ya Rombo
	<ul style="list-style-type: none"> • Kazi za miradi zenye thamani ya Sh.91,448,907.77 hazikukamilika au hazikutekelezwa.
32	Halmashauri ya wilaya ya Kilwa
	<ul style="list-style-type: none"> • Kazi za miradi zenye thamani ya Sh.91,103,556 hazikukamilika. • Sh. 231,795,182.50 zilizotumika hazikuandaliwa taarifa za utekelezaji wa miradi. • Hakuna uthibitisho endapouhamisho wa kiasi cha Sh.25,277,838 kwenda Akaunti mbalimbali za vijiji kama fedha hizo ziliwafikia walengwa.

33	Halmashauri ya wilaya ya Liwale
	<ul style="list-style-type: none"> • Akauti ya kijiji ilipatiwa Sh. 40,351,240 kwa ajili ya kazi za miradi lakini miradi haikutekelezwa. • Kazi za miradi zenye thamani ya Sh. 65,194,178 hazikukamilika.
34	Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa
	<ul style="list-style-type: none"> • Kazi za miradi zenye thamani ya Sh.271,015,787 hazikukamilika. • Akauti ya kijiji ilipatiwa Sh.82,438,300 kwa ajili ya kazi za miradi saba lakini miradi hiyo haikutekelezwa. • Hapakuwa na stakabadhi za kukiri uhamisho wa kiasi cha Sh.20,785,050 kwenda kwenye akaunti za vijiji mbalimbali.
35	Halmashauri ya wilaya ya Mafia
	<ul style="list-style-type: none"> • Mradi wa ufugaji kuku usioendelevu katika kijiji cha Chole uligharimu Sh.8,790,000 • Miradi yenye thamini ya Sh.69,493,600imekamilika lakini ilikuwa na dosari mbalimbali.
36	Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo
	<ul style="list-style-type: none"> • Kutokukamilika ujenzi wa jengo la utawala Shule ya sekondari Zinga. • Malipo ya kushughulikia usimamizi wa maendeleo ya mradi yalilipwa kimakosa toka kwenye mfuko wa kijiji (NVF) - Sh.11, 524,390
37	Halmashauri ya wilaya ya Kibaha
	<ul style="list-style-type: none"> • Nishati ya jua haijafungwa katika jengo la zahanati ingawa ujenzi umekamilika.
38	Halmashauri ya wilaya ya Kisarawe
	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa soko la Mzenga 'A' wenye thamani ya Sh.32,640,182.50 halikuzingatia michoro iliyopitishwa. • Sh. 30,977,221.50 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu. Miaka mitatu imepita bila ujenzi huu kukamilika hii ni kinyume na taratibu zilizowekwa na TASAF.
39	Halmashauri wilaya ya Rufiji
	<ul style="list-style-type: none"> • Katika kijiji cha Ngorongo Madarasa matatu na tanki la kuhifadhia maji yamejengwa chini ya kiwango thamani ya mradi huu ni Sh. 8,142,562 • Ujenzi wa maabara ya shule ya sekondari Ruaruke wenye thamani ya Sh. 19,700,827 haujakamilika.
40	Halmashauri ya wilaya ya Biharamulo
	<ul style="list-style-type: none"> • Madawati yenye thamani ya Sh 270,000 hayajapokelewa.
41	Halmashauri ya wilaya ya Muleba
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri haikuandaa bajeti kwa ajili ya miradi. • Dosari mbalimbali zilizoonekana wakati wa ujenzi wa choo cha

	shimo thamani ya mradi Sh.31,508,100
42	Manispaa ya Shinyanga
	<ul style="list-style-type: none"> • Kazi za miradi zenye thamani ya Sh.60,259,500 hazikukamilika. • Menejimenti ya manispaa haijachukua hatua kwa ajili ya miradi miwili isiyo endelevu. Kutokana na hali hii jamii haijapata huduma iliyoitegemea.
43	Halmashauri ya wilaya ya Bukoba
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri haijajibu hoja za miaka ya nyuma zilizotolewa na wakaguzi Sh. 215,783,722.06. • Ujenzi wa zahanati tatu (3) wenye thamani ya Sh.35,213,254.54 umekamilika lakini hazijaanza kutoa huduma kwa jamii. • Ujenzi wa soko la Katoma haujakamilika Sh.8,861,500.
44	Manispaa ya Tabora
	<ul style="list-style-type: none"> • Miradi yenye thamani ya Sh. 346,725,451 sawa na asilimia ishirini na saba (27%) ya fedha zilizopokelewa hazijakamilika. • Ujenzi wa nyumba ya muuguzi zahanati ya Lusangi wenye thamani ya Sh.37, 373,130 haujakamilika. • Ujenzi wa madarasa matatu(3) Shule ya sekondari Tumbi wenye thamani ya Sh. 49,929,779 haujakamilika. • Mradi wenye thamani ya Sh.10,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya usindikaji mbegu haujakamilika.
45	Halmashauri ya wilaya ya Manyoni
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri ilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh.5,340,000 bila kushindanisha wazabuni. • Manunuzi yenye thamani ya Sh.3,374,800 yalifanywa bila idhini ya bodi ya manunuzi.
46	Halmashauri ya wilaya ya Bahi
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh.186,466,772 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya TASAF zilipokelewa mwishoni mwa mwaka wa fedha. • Kiasi cha Sh.8,225,000 kililipwa kwa Mkugenzi wa Halmashauri (DED) badala ya kulipwa mhusika. • Mpango wa mwaka wa manunuzi kwa ajili ya miradi haukuandaliwa.
47	Halmashauri ya wilaya ya Nzega
	<ul style="list-style-type: none"> • Kazi za miradi zenye thamani ya Sh.4,192,000 hazikukamilika.
48	Halmashauri ya wilaya ya Urambo
	<ul style="list-style-type: none"> • Sh.39,203,560 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu; bado mradi huo haujatekelezwa.
49	Halmashauri ya wilaya ya Chamwino
	<ul style="list-style-type: none"> • Miradi yenye thamani ya Sh.181,083,031.82 ilikuwa kwenye hatua za mwanzo.

50	Halmashauri ya wilaya ya Igunga
	<ul style="list-style-type: none"> Bidhaa ambazo hazikuingizwa kwenye daftari la kumbukumbu ya manunuzi-Sh.5,648,600 <p>Kulikuwa na mapungufu katika utayarishaji wa Taarifa ya fedha.</p>
51	Halmashauri ya wilaya ya Kondoa
	<ul style="list-style-type: none"> Kazi za miradi zenye thamani ya Sh.191,885,060 hazikukamilika. Uchelewes haji wa utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh.23,300,000 katika kijiji cha Gwandi.
52	Halmashauri ya wilaya ya Sikonge
	<ul style="list-style-type: none"> Halmashauri haikutekeleza hoja/mapendekezo ya miaka iliyopita yaliyotolewa na wakaguzi.
53	Halmashauri ya wilaya ya Sengerema
	<ul style="list-style-type: none"> Taarifa ya fedha inayoishia tarehe 30.6.2012 ilionyesha marekebisho Sh.34,816,000 yaliyofanywa bila kutolewa maelezo. Matumizi ya kiasi cha Sh. 5,650,000 yalilipwa kwenye vufungu visivyohusika Kiasi cha Sh.31,574,894.76 kiliamishiwa kwenye akaunti za miradi ya jamii lakini wahusika hawakukiri kupokea fedha hizo. Sh.5,090,000 sawa na 2.5% kwa ajili ya fedha za kusimamia shughuli za miradi vijiji zilikapwa na Mkurugenzi wa Halmashauri (DED) hazijarejeshwa. Halmashauri haijachangia kiasi cha Sh.23,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya TASAF.
54	Halmashauri ya wilaya ya Masasi
	<ul style="list-style-type: none"> Malipo ya kiasi cha Sh. 3,340,000 hayakuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo namba 5(c) la Memoranda ya Fedha Mamlaka za Serikali za Mitaa mwaka 1997. Halmashauri ilibadilisha (aina) utekelezaji wa miradi ya jamii(CMC projects) yenye thamani ya Sh.44,925,934.01 bila idhini ya TASAF makao makuu. Halmashauri ililipa Sh.5,992,700 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya magari. Hata hivyo namba za usajili wa magari yaliyotumika katika usimamizi wa miradi hazikuweza kutolewa kwa ajili ya uhakiki.
55	Halmashauri ya wilaya ya Nanyumbu
	<ul style="list-style-type: none"> Matumizi ya mafuta ya magari kiasi cha lita 396 yenye thamani ya Sh.904,000 hayajahakikiwa. Mbuzi 34 wenye thamani ya Sh.2,380,000 wa mradi wa kijiji cha Kamundi walikufa. Jamii haijapata faida kutokana na mradi huu. Miti 96 yenye thamani ya Sh.3,390,000 iliyopandwa kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo nane vya maji ilikauka kwa ajili ya ukame.

56	Manispaa ya Iringa
	<ul style="list-style-type: none"> • Kulikuwa na bakaa ya Sh.123,138,595 sawa na 71.7%; kiasi hiki kilitokana na Sh.171,963,062 zilizopokelewa na halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.Utekelezaji wa miradi haukukamilika kwa sababu ya ucheleweshaji wa fedha. • Ujenzi wa choo cha shule ya sekondari Tagamenda wenye thamani ya Sh. 11,972,773 ulikuwa chini ya kikwango. • Kulikuwa na tofauti ya kiasi cha Sh.153,901,493 kwenye ruzuku ya maendeleo.
57	Jiji la Mbeya
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri ilipokea fedha pungufu ya iliyoidhinishwa kwa kiasi cha Sh.217,183,820 • Miradi ya thamani ya Sh. 92,843,000 haikukamilika. • Miradi ya thamani ya Sh. 40,282,000 ilikamilika lakini haijaanza kutumika.
58	Halmashauri ya wilaya ya Mbinga
	<ul style="list-style-type: none"> • Ucheleweshwaji wa Taarifa ya fedha kwa ajili ya ukaguzi. • Mapendekezo ya ukaguzi ya mwaka uliopita hayajatekelezwa-Shs.1,990,300.
59	Halmashauri ya wilaya ya Mpanda
	<ul style="list-style-type: none"> • Miradi ya thamani ya Sh.203,501,944 haikukamilika. • Matumizi ya fedha zilizohamishiwa kwenye akaunti za maendeleo ya miradi Sh.143,376,768 hayakuainishwa.
60	Halmashauri Wilaya ya Iringa
	<ul style="list-style-type: none"> • Miradi ya thamani ya Shs. 209,308,071 haikukamilika. Fedha iliyotengwa kwa ajili ya kukamilisha mradi inaweza isitoshe kutokana na uwezekano wa vifaa vitakavyotumika kupanda bei.
61	Halmashauri ya wilaya ya Kilolo
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh.1,189,000 kililipwa kwa ajili ya matengenezo ya magari lakini taarifa ya hali ya magari baada au kabla ya matengenezo ya magari haikuwasilishwa.
62	Halmashauri ya wilaya ya Sumbawanga
	<ul style="list-style-type: none"> • Sh.30,723,062 zilizohamishiwa kwenye miradi ya jamii kwa ajili ya utekelezaji wa miradi haikuingizwa kwenye taarifa ya hesabu.

	<ul style="list-style-type: none"> • Taarifa ya mtiririko wa fedha ilionyesha kwenye bakaa ya fedha taslimu kulikuwa na upungufu wa Sh.30,723,062 • Kasoro mbalimbali zilijitokeza kwenye mradi wa ujenzi wa vyoo vya mashule na zahanati wenye thamani ya Sh.17,402,600. • Miradi ya thamani ya Sh.5,325,505 haikukamilika.
63	Halmashauri ya wilaya ya Ludewa
	<ul style="list-style-type: none"> • Bajeti ya halmashauri haikupata kibali cha utekelezaji wa miradi ya TASAF yenye thamani ya Sh.17,072,905.
64	Halmashauri ya wilaya ya Makete
	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa soko la Mfumbi haukukamilika kwa sababu ya ukosefu wa meza za kuuzia.Badala yake Jamii inatumia eneo hili kuuzia pombe za kienyeji bila ya kibali cha kamati.Utumiaji wa soko kabla ya kukamilika utasababisha uharibifu.
65	Halmashauri ya wilaya ya Mbeya
	<ul style="list-style-type: none"> • Miradi ya TASAF II haikupitiwa na kamati ya ukaguzi ya halmashauri. • Hati za malipo ya kiasi cha Sh. 8,630,000 hazikuwasilishwa • Mali zenye thamani ya Sh.1,669,500 hazikuingizwa katika leja • Manunuzi kiasi cha Sh.2,900,000 yalifanyika nje ya mpango wa manunuzi.
66	Halmashauri ya wilaya ya Mufindi
	<ul style="list-style-type: none"> • Mpango wa utekelezaji wa miradi ya TASAF ulifanyika baada ya kupokea fedha kiasi cha Sh.13,202,448.
67	Halmashauri ya wilaya ya Songea
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo ya kiasi chaSh. 1,530,000hayakuwa na nyaraka za kutosha. • Malipo ya Sh.1,290,000 hayakuhakikiwakabla ya malipo.
68	Halmashauri wilaya ya Rungwe
	<ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri inashauriwa iliingize gari (STK 2123 - Land Rover) kwenye taarifa ya fedha katika jedwali la mali za kudumu (mitambo, mali na vifaa).
69	Halmashauri ya wilaya ya Geita
	<ul style="list-style-type: none"> • Taarifa linganifu iliripoti Uchakavu wa mali kwa upungufu wa Sh.154,935,000. • Taarifa ya fedha ilizidisha ruzuku kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa kiasi cha Sh.1,420,000
70	Halmashauri ya wilaya ya Misenyi
	<ul style="list-style-type: none"> • Fedha kwa ajili ya Maendeleo ya ruzuku ilizidishwa kwa kiasi cha Sh.4,382,730.

71	Halmashauri ya wilaya ya Simanjiro
	<ul style="list-style-type: none"> Ruzuku ya maendeleo Sh.684,271,022 iliwasilishwa kwenye taarifa ya fedha kama ruzuku kwa ajili ya matumizi ya kawaida Miradi ya thamani ya Sh. 298,001,427 haikukamilika.
72	Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa
14	Mradi wa Maendeleo ya Biashara na Usafirishaji Kanda ya Afrika ya Mashariki-SUMATRA
15	Programu ya Uzalishaji katika Kilimo Afrika ya Mashariki-APL 1
16	Programu ya Kanda Miundombinu ya Mawasiliano
17	Mradi wa Ubunifu uliowazi katika Tasinia ya uchimbaji madini Tanzania-TEITE
18	Mradi wa Ubunifu uliowazi katika Tasinia ya Uchimbaji Madini Tanzania-TEITE Grant no.96777
19	Mradi wa Kuhifadhi Chakula vijijini
20	Kituo cha Mafunzo cha Kimataifa Kupitia Mtandao wa Kompyuta (TGDL)
21	TZ-Agr Sec Dev (FY06)(ASDP) - PMO - RALG
22	Mradi wa Kusaidia Programu ya Sekta ya Afya-Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
23	Programu ya Usafirishaji Serikali za Mitaa na Vijijini
24	Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo- PMO-RALG Component
25	Wakala wa Nishati Vijijini-Mradi wa Maendeleo

26	Mradi Wa Msaada WaKupunguzaVifo Vya Wajawazito P-Tz- IBO - 001
27	Mradi wa Kukopesha Wajasiriamali wadogo Awamu ya II(SELF)
28	Mradi wa Barabara ya Singida - Babati -Minjingu
29	Mradi wa Makumbusho ya Kitaifa na Nyumba ya Utamaduni
30	Sida/NORAD/MEM -Mradi wa nishati ya mimea
31	Mradi wa Kuwezesha Biashara na Usafirishaji kanda ya Afrika Mashariki
32	Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma (PSRP) Mfuko mkuu-Hazina
33	Programu ya Maboresho Serikali za Mitaa -Mfuko mkuu (LGRP)
34	Mfuko Mkuu maboresho ya kisasa ya ukusanyaji kodi
35	Mfuko Mkuu wa Sekta ya Maji
36	Mfuko Mkuu wa Kitaifa wa Usambazaji Maji Safi Vijijini
37	Mfuko Mkuu wa Huduma za Afya
38	Mfuko Mkuu sekta ya Sheria
39	Mfuko Mkuu wa Sera yarasilimali watuya Mpango wa Maendeleo(PHRD) Kuendeleza Sekta ya Kilimo
40	Mfuko Mkuu katika kutoa msaada sekta ya fedha
41	Mfuko Mkuu -Mpango wa elimu shule za Sekondari
42	Mfuko mkuu wa STATCAP
43	Mfuko Mkuu programu ya maendeleo shule za sekondari

44	Program ya maendeleo Umoja wa Mataifa -Ofisi ya Makamu wa Raisi (UNDP)
45	Program ya maendeleo Umoja wa Mataifa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Raisi Zanzibar (UNDP)
46	Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (UNDP)
47	Huduma ya Kimataifa Idadi ya Watu (UNDP)
48	Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Raisi Zanzibar (UNDP)
49	Ofisi ya Taifa yaTakwimu (UNDP)
50	Mamlaka ya Chakulana DawaTanzania (UNDP)
51	Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii (UNDP)
52	Wakala wa Usajiri wa Vifo na Uzazi na Udhhamini (UNDP)
53	Wizara ya ElimunaMafunzo ya Ufundi--Zanzibar(UNDP)
54	Wizara ya AfyanaUstawi wa Jamii-Mazingira ya Afya (UNDP)
55	Wizara yaUstawi wa Jamii,Vijana, Wanawake naMaendeleo ya Watoto -Zanzibar (UNDP)
56	Wizara ya ElimunaMafunzo ya Ufundi (UNDP)
57	ElizabethGlaserkwa WatotoUKIMWIFoundation, (UNDP)
58	Ofisiya Makamu wa RaisBaraza la Taifala Usimamizi wa Mazingira(UNDP)
59	Hudumia watoto (UNDP)
60	Chama chaMadaktari Wanawakewa Tanzania (MEWATA)(UNDP)
61	Halmashauri ya Wilaya ya Makete -(UNDP)

62	Ofisi ya Waziri Mkuu (UNDP)
63	Mfuko wa Mimitu Tanzania - TFS (UNDP)
64	Wizara ya Maji (UNDP)
65	Wizara ya Mendeleo ya Mifugo na Uvuvi (UNDP)
66	Mama2mama (UNDP)
67	Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania (UNDP)
68	Mfuko wa Kimataifa wa kupambana na UKIMWI Kifua Kikuu na Ukoma kwa ajili ya Wizaraya Ustawi wa Afya na Ustawi

- (b) **Miradi yenye Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo** lfuatayo ni Miradi ya maendeleo ishirini na mbili (22) iliyopata hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo na sababu zake zimeonyeshwa kwenye jedwali Na.43 hapa chini:

Jedwali 43: Miradi yenye Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo

1	TZ-Loc Govt SIL (FY 05) -PMO-RALG & DAR PST
	<ul style="list-style-type: none"> Kulingana na taarifa za Benki ya Dunia kiasi cha mkopo uliosainiwa ni dola za kimarekani 103,348,091.00 ambapo kiasi kilichokwishaletwa ni dola za Marekani 100,143,474.23 hivyo kiasi cha dola za Marekani 3,204,616.77 hakijaletwa ikiwa ni sawa na Sh. 5,000,000,000. Thamani ya mkopo itakayolipwa ni kiasi cha dola za Marekani 100,143,474.23 na siyo dola za Marekani 103,348,091.00 zilizo sainiwa.
2	Mradi wa mabasi yaendayo kasi DAR (DARTS)
	<ul style="list-style-type: none"> Wakala ilitumia kiasi cha Sh.169,381,739 kulipa posho ambazo hazikuwa na kibali cha bodi ya Ushauri na hakikuonyeshwa kwenye bajeti ya Wakala kwa mwaka wa fedha 2011/12. Wakala ilitayarisha orodha ya malipo ya kiasi Sh.8,790,162,620 kwa ajili fidia kwa watu wa Gerezani walio athirika na mradi ambapo taarifa ya mthamini wa

	Serikali iliyoidhinishwa inaonyesha malipo ya fidia ya kiasi cha Sh.2,620,488,000 kwa watu wale wale.
3	Ukarabati wa Miundombinu ya Afya ya Wilaya TAMISEMI- kipengele
	<ul style="list-style-type: none"> Taarifa ya fedha haikuonesha madeni ya kiasi cha Sh.43,807,500 na wala hakuna bajeti ya madeni haya katika mwaka wa fedha 2011/2012
4	Mradi wa Mtandao wa Afya ya Umma Afrika Mashariki IDA Credit Number 47310
	<ul style="list-style-type: none"> Kiasi cha Sh. 3,634,121,925 ikiwa sawa na asilimia 86.2 ya fedha yote hakikutumika, hivyo kazi za mradi zilizokuwa zimeainishwa kwenye bajeti hazikutekelezwa kama ilivyokuwa imekusudiwa.
5	Mradi wa rasilimali/ kitega uchumi Wilayani Sekta ya Kilimo (DASIP)
	<ul style="list-style-type: none"> Kiasi cha fedha Sh. 9,775,000 kilichopelekwa Halmashauri za Wilaya za Misungwi na Geita pia kiasi cha Sh.31,896,000 kwa ajili ya kununua pikipiki na kulipa posho za watumishi hazikuonekana katika taarifa za benki. Hadi kufikia Septemba 2012 kulikuwa na kazi za mradi ambazo hazijatekelezwa za kiasi cha Sh.1,495,173,000.
6	Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency
	<ul style="list-style-type: none"> Uwezekano wa kuendelea kuwepo kwa wakala ni wa mashaka kwani washirika maendeleo hawajatekeleza mkakati endelevu kulingana na kifungu 24.2 (CCTTFA) cha mkataba endapo msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika utafikia kikomo.
7	Local Government Support Project IDA Credit No. 4003
	<ul style="list-style-type: none"> Kulingana na taarifa ya benki ya Dunia kiasi cha mkataba uliosainiwa ni dola za Marekani 103,348,091.00 ambapo mkopo uliokwisha kutolewa ni dola za Marekani 100,143,474.23 hivyo kiasi ambacho hakijatolewa ni dola za Marekani 3,204,616.77 ikiwa sawa Sh. 5,000,000,000. Kiasi cha mkopo wa dola za Marekani 100,143,474.23 ndicho kitakacholipwa na siyo kiasi cha dola za 103,348,091.

8	The Second Centre Transport Corridor Project Credit No. 4455
	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchelewa kuanza kwa kazi kwani TANROADS wameshindwa kukabidhi maeneo ya kazi kwa mkandarasi Jangwani Bridge, City Council Station, Ubungo bus terminal, Kimara Terminal. • Kuchelewa kuanza kwa Package2- inayohusu ujenzi wa Ubungo Depot, Ubungo Feeder station na kituo cha mabasi yaendayo mikoani kwa mkataba wa Sh.2,201,086,467.Mkataba Na. TRD/HQ/1020/2011/12 ulisainiwa tarehe 9/8/2010 kati ya TANROAD na Beijing Construction Engineering Group Co lakini hadi Novemba 2012 kazi zilikuwa bado hazijaanza. • Kuchelewa kuanza kwa Package 5- inayohusu ujenzi wa Kariakoo Terminal and Feeder station- bei ya mkataba na TRD/HQ/1012/2010/11 ni kiasi cha Sh.6,348,331,889.Mkataba ulisainiwa tarehe 9/8/2010 kati ya TANROADS lakini bado utekelezaji wa kazi za mkataba haujaanza. • Makandarasi China Civil Engineering ameleta madai ya fidia ya kiasi cha Sh.174,573,138 kwa sababu ya ucheleweshaji wa kazi za mkataba kwa miezi saba kuanzia katika sehemu ya wazi Jangwani malipo hayo yanaonekana kama serikali haikupata manufaa.
9	TZ-Strategic Cities Project
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo ya kiasi cha Sh.6,277,500 kwa ajili ya safari ya Kigoma - Morogoro - kigoma yalikuwa siyo ya lazima na hakuna vielelzo vya matumizi ya kukodi gari kwa washiriki kutoka Kigoma kwenda Dar es salaam (Ubungo Bus Stand) kujifunza namna ya kukusanya maduhuli katika kituo cha mabasi na pia kutoka Kigoma kwenda Morogoro kujifunza kuhusu taka ngumu katika halmashauri ya manispaa ya Morogoro.
10	Road Sector Support Project I (RSSPI)
	<ul style="list-style-type: none"> • Utekelezaji mdogo wa barabara ya Namtumbo - Tunduru (193 km). Ni dhahiri kwamba mkandarasi ameshindwa kutekeleza mkataba hivyo, wakala wa barabara (TANROAD) ina kusudia kuvunja/kusitisha maktaba.

11	Rural Water Supply and Sanitation program II (water Sector Component) (RWSSP)
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha fedha Sh.4,870,000 hakikutumika kutekeleza miradi inayohusu RWSSP. • Menejimenti ya PMO RALG's ilipokoea hati ya madia ya kiasi cha Sh.7,137,767 kabla ya kutoa hatia ya kuagiza huduma/vifaa (LPOs)
12	Market, Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support Programme (MIVARF)
	<ul style="list-style-type: none"> • Mradi ulipokea kiasi cha Sh.9,590,878,253.80 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hata hivyo ni kiasi cha Sh. 3,654,443,543.19 ndio kilitumika ikiwa sawa na asilimia 38 na bakaa ya kiasi cha Sh. 5,935,194,119 ikiwa sawa na asilimia 62 haijatumika.
13	The private Sector Competitiveness Project (PSCP) Component 2 Enterprise Development Under The TZ Private Sector Foundation IDA CREDIT NO, 4136
	<ul style="list-style-type: none"> • Baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa vya thamani ya dola za Marekani 626,521.67 havijatumika
14	TZ: Accelerated Food Security Project
	<ul style="list-style-type: none"> • Kulikuwa na hati za malipo batili za kiasi cha Sh 159,620,000 zilitakiwa kulipwa • Kulikuwa na hati za malipo za kiasi cha Sh.407,440,000 ambazo siyo sahihi • Utekelezaji wa mkataba zaidi ya makubaliano kiasi cha Sh.40,802,000.
15	Teaching and Learning Science ,Mathematics and English in Government Secondary Schools in Project using ICT
	<ul style="list-style-type: none"> • Mradi haukuandaa daftari la fedha na taarifa za usuluhishi wa benki hivyo, taarifa za fedha zimeonyesha salio ishia la kiasi cha Sh.64,544,304 ambapo taarifa za benki zinaonyesha salio ishia kiasi cha Sh.95,008,908.
16	TZ-Marine & Costal Env Mgmt SIL (FY06) -TZ Mainland & Zanzibar - GEF (MACEMP)
	<ul style="list-style-type: none"> • Matumizi batili kiasi cha Sh.124,776,801 ikiwa ni malipo ya kodi ya ongezeko (VAT) • Maeneo ya mialo ya uvuvi yamekamilika lakini hayatumiki katika sehemu zifuatazo: <ul style="list-style-type: none"> i) Kilwa Masoko Pwani imegharimu kiasi cha

	<p>Sh.155,444,025.</p> <p>ii) Nyamisati imegharimu kiasi cha Sh.125,008,848.08</p> <ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi uliotumia kiasi cha Sh.263,824,666 haukukamilika na uko chini ya kiwango katika sehemu za Tumbe, Pemba. • Mfuko wa urithi wa baharini haujaanzishwa (Marine Legacy Fund).
17	Lake Victoria Environmental Project (LVEMPII)
	<ul style="list-style-type: none"> • Utekelezaji mdogo wa mkataba wa huduma ya ushauri na ME-011/2011/2012 wa tarehe 24 Januari, 2012 kwa ajili ya kubuni na kusimamia ujenzi wa mfumo wa maji taka katika eneo la Mabatini Igogo jiji la Mwanza. Mkataba alipewa mkandarasi Beomhan Engineering and Architects Co Ltd kwa kushirikiana na DOCH Engineering and Management consultants wa sanduku la posta 1767 DSM kwa mkataba wa Sh.77,809,000 kwa kipindi cha wiki 12 kuanzia tarehe 1/4/2012 hadi 30/12/2012. Utekelezaji wa mkataba haujakamilika hadi leo. • Miradi ya kiasi cha Sh.109,206,137 haijakamilika: <ul style="list-style-type: none"> - Ununuzi wa mashine ya dizeli ya thamani ya Sh.41,206,137 katika kijiji cha Sunguti haujafanyika - Ukarabati wa bwawa la maji lenye thamani ya Sh.32,000,000 katika kijiji cha Bubinza, Wilaya ya Magu haujakamilika. - Ujenzi wa bwawa la maji lenye thamani ya Sh.36,000,000 katika kijiji cha Mwamkale wilaya ya Magu haujakamilika.
18	Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Afya -mzunguko wa Tisa (9) (HSSGFR9).
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh. 4,435,531,639.28 ikiwa ni sawa na asilimia 36 ya fedha yote ilikuwa haijatumika hivyo, kazi za mradi hazikutekelezwa kama ilivyokusudiwa.
19	Mradi wa ufuatiliaji na tathimini- Mzunguko wa nane (8) (MEGFR8)
	<ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha Sh. 58,774,401 ikiwa ni sawa na asilimia 57 ya fedha yote ilikuwa haijatumika hivyo, kazi za mradi hazikutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

20	Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Pwani na Baharini (MACEMP) IDA Credit No. 4106
	<ul style="list-style-type: none"> Malipo yasiyo kuwa ya kawaida na kutomalizika kwa nyumba ya Mvuvi (Mvuvi House) <p>Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi iliingia mkataba namba 31 wa mwaka 2009/2010 na CATIC International Engineering (T) Ltd, Box 11600, Dar es Salaam kujenga jengo la ofisi la ghorofa tatu kwa bei ya mkataba wa kiasi cha Sh.3,534,145,946.40. Mkataba ulisainiwa tarehe 26/2/2010 kwa kipindi cha miezi nane hivyo ilitakiwa kukamilika mwezi Novemba, 2010. Katika mwaka huu kiasi cha Sh.1,132,212,322.59 kililipwa kwa mkandarasi CATIC International Engineering (T) Ltd.</p>
21	Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti UKIMWI (NACP) - Mzunguko wa nane (8)
	Malipo ya kiasi cha Sh.1,109,746,805 hayakuwa na viambatisho vya kutosha kinyume na kanuni 95(4) ya Sheria ya Fedha Za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekibishwa mwaka 2004).
22	National Multi - Sectoral Framework (NMSF)
	Hati za malipo ya kiasi cha Sh.8,689,997 yalionyeshwa kwenye kasima ya matumizi isiy sahihi kinyume na Kanuni ya 49(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2005

(C) Miradi iliyopata hati zenye shaka

Miradi mitatu (3) ilipata hati yenye shaka kama inavyoonekana kwenye jedwali 44 hapa chini:

Jedwali 44: Miradi iliyopata hati yenye shaka

1	Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)- UNDP
	<ul style="list-style-type: none"> Menejimenti ya Tume ya kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) ilionyesha mapungufu katika kusimamia miradi ambapo hadi Mei 2012 miradi minne ya huduma ya ushauri ya kiasi cha Sh.20,800,000 haikukamilika katika muda wa mkataba kwa ucheleweshaji wa siku sitini na moja. Tofauti ya kiasi cha Sh. 288,381,371.95 kati ya fomu za FACE na daftari la fedha Tofauti ya kiasi cha Sh 75,000,000 kati ya taarifa ya fedha salio anzia na kiasi kilichopokelewa na pia

	jumla ya matumizi yalionyeshwa kiasi cha Sh.milioni 171 badala ya Sh.milioni 103
2	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo ya kiasi cha Sh.100,904,500 hayakuwa na viambatisho • Malipo ya kiasi cha Sh.71,715,000 hayakuwa na viambatisho ili kuthibitisha uhalali wake. • Dosari katika taarifa za fomu za FACE, matumizi yaliyoonyeshwa kwenye mtandao wa Epicor na taarifa za kila mwezi za mradi. Halmashauri ilionyesha kiasi cha matumizi ya Sh.582,226,000 katika fomu za FACE, taarifa za maendeleo ya kazi kiasi cha Sh.258,072,500 na mfumo wa kompyuta wa Epicor ilionyesha kiasi cha Sh. 623,946,000 . Hivyo, ukaguzi umeshindwa kuthibitisha usahihi wa matumizi kwa taarifa za fedha zinazoishia tarehe 31 Disemba 2011
3	Wizara ya Madini na Nishati
	<ul style="list-style-type: none"> • Hati za malipo za kiasi cha Dola za kimarekani 493,941.52 na viambatisho vyake havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Januari 2011 hadi 31 Disemba 2011.

SURA YA TANO

MAPITIO YA TARATIBU NA MIKATABA YA MANUNUZI

5.0 Utangulizi

Katika kipindi cha ukaguzi wa taarifa za fedha za miradi ya maendeleo mwaka 2011/2012, nilibaini mapungufu katika manunuzi ya huduma na vifaa yaliyofanyika Mfuko wa Huduma za Jamii, programu ya maendeleo sekta ya kilimo, programu ya mradi wa maendeleo ya sekta ya maji, mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Afya na miradi mingine ya maendeleo. Mapungufu yaliyobainika yalitokana kwa kiasi kikubwa na kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2004 na Kanuni zake za mwaka, 2005 kama ilivyoonyeshwa hapa chini.

5.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo

5.1.1 Manunuzi ya mali na vifaa bila kuingizwa kwenye daftari Sh.22,018,512.50

Kumbukumbu kwa ajili ya matumizi ya vifaa hazikutunzwa hivyo haikuwa rahisi kuchunguza matumizi ya vifaa hivyo. Pia matumizi ya vifaa vyenye thamani ya Sh.22,018,512.50 hayakuweza kubainika. Katika mapitio ya manunuzi ilibainika kuwa Halmashauri saba(7) hazikuingiza vifaa zilizonunua kwenye daftari. Mchanganuo wa Halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 45 hapa chini:-

Jedwali Na. 45: Mali na vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari

Na	Halmashauri	Kiasi (Sh)
1	Kyela	6,171,800.00
2	Nachingwea	4,472,217.50
3	Kahama	3,149,895.00
4	Kilosa	2,802,500.00
5	Hanang	2,752,100.00
6	Arusha	1,710,000.00
7	Mafia	960,000.00
	Jumla	22,018,512.50

Hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali bila kugundulika.

**5.1.2 Mali na Vifaa Vilivyonunuliwa bado havijapokelewa
Sh. 76,546,863**

Mali na vifaa vya thamani ya Sh.76,546,863 vilivyonunuliwa kwa kutumia fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo havijapokelewa. Hii ni kinyume na Agizo Na.71(b) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Mchanganuo wa Halmashauri nane (8) zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 46 hapa chini:

**Jedwali 46: Mali na Vifaa Vilivyonunuliwa bado
Havijapokelewa**

	Halmashauri	Kiasi (Sh)
1	Chato	4,000,000
2	Ileje	18,000,000
3	Manyoni	11,415,000
4	Mbulu	855,000
5	Meatu	18,750,000
6	Mtwara	152,863
7	Mwanza	4,708,000
8	Tarime	18,666,000
	Jumla	76,546,863

**5.1.3 Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi ya zabuni
Sh.270,102,712**

Manunuzi mengi yaliyofanywa kwa mkataba yalikuwa na mapungufu mengi. Hii inatokana na usimamizi mbovu wa mikataba. Ilibainika kuwa Halmashauri saba (7) zilifanya manunuzi ya kiasi cha Sh.270,102,712.00 bila idhini ya Bodi ya zabuni hii ni kinyume na kanuni Na. 40 na 41 ya Kanuni za manunuzi ya umma, 2005. Mchanganuo wa Halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 47 hapa chini:-

**Jedwali 47: Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi ya
zabuni**

Na	Halmashauri	Kiasi (Sh)
1	Chamwino	40,629,617
2	Mkuranga	50,976,000

3	Manispaa ya Mtwara	23,610,000
4	Mufindi	27,308,068
5	Muleba	60,886,527
6	Rorya	61,912,500
7	TAMISEMI	4,780,000
Jumla		270,102,712

5.1.4 Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha Wazabuni Sh.252,937,907

Halmashauri nane (8) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh.252,937,907 bila kushindanisha wazabuni. Hii ni kinyume na Kanuni ya 28 ya Kanuni za manunuzi ya umma,2005. Mchanganuo wa Halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 48 hapa chini:-

Jedwali 48:Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanishwa

Na	Halmashauri	Kiasi (Sh)
1	Arusha MC	1,829,000
2	Babati DC	7,462,600
3	Chamwino DC	49,273,662
4	Kinondoni MC	30,045,632
5	Kongwa DC	13,600,000
6	Masasi DC	98,640,700
7	Shinyanga MC	1,884,500
8	Urambo DC	50,201,813
Jumla		252,937,907

5.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya

5.2.1 Mali na vifaa vya thamani ya Sh.180,703,985 havijapokelewa

Mali na vifaa vya thamani ya SH. 180,703,985 vilivyounuliwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Afya havijapokelewa kinyume na Kanuni 122 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2005 inayosisitiza uwepo wa taarifa ya kupokea vifaa kwanza na baadaye malipo kuidhinishwa. Angalia jedwali namba 49.

Jedwali 49:Mali na vifaa ambavyo havijapokelewa

Na	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Manispaa ya Kinondoni	30,858,300
2	Magu	2, 875,200
3	Kwimba	5,000,000
4	Jiji la Mwanza	109,101,100
5	Hanang	4,185,000
6	Mji wa Babati	28,684,385
	Jumla	180,703,985

5.2.2 Manunuzi ya Dawa na vifaa vya tiba kutoka kwa wazabuni binafsi bila kibali cha Bohari Kuu ya Dawa Sh.412,219,600

Kiasi cha Sh 412,219,600 kililipwa ikiwa ni manunuzi ya Dawa na vifaa vya tiba kwa wazabuni binafsi bila kibali cha Bohari Kuu ya Dawa kinyume na kifungu 3.5 (h) sura ya tatu Mwongozo wa Mkakati Maalumu wa Afya kwa Halmashauri wa mwaka, 2007. Halmashauri (10) zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 50 hapa chini:

Jedwali 50:Manunuzi bila kibali cha Bohari Kuu ya Dawa

Na	Halmashauri	Kiasi (Sh)
1	ya Manispaa Ilala	127,183,300
2	Kilosa	62,600,630
3	Ulanga	14,769,000
4	Mji wa Kibaha	27,363,530
5	Magu	4, 740,000
6	Kwimba	11,900,000
7	Jiji la Mwanza	71, 806,500
8	Manispaa ya Arusha MC	47,570,500
9	Simanjiro	14,678,500
10	Tandahimba	29,510,000
	Jumla	412,219,600

5.2.3 Ununuzi wa mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bodi ya Zabuni Sh.121,391,503

Kanuni Na. 68(5) ya kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2005, inaagiza kwamba kuwepo na orodha ya wauzaji waliopendekezwa na Bodi ya Zabuni na hatimaye Taasisi inayofanya ununuzi itaandaa maombi ya kwa njia ya dodoso za ununuzi kwa wauzaji wote waliochaguliwa. Hata hivyo, Halmashauri sita(6) zilikiuka kanuni Na.68(5) ya Kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2005 kwa kufanya ununuzi wa mali, kazi za ujenzi na kazi zisizo za ushauri kutoka kwa wauzaji ambao hawakuthibitishwa na Wakala we jedwali Na 51 hapa chini:

Jedwali 51: Ununuzi wa mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bodi ya Zabuni

Na	Halmashauri	Kiasi (Sh)
1.	Kibondo	5,277,000
2	Nzega	56,159,000
3	Kyela	18,124,250
4	Mbarali	4,223,500
5	Rombo	8,992,753
6	Kilwa	28,615,000
	Jumla	121,391,503

5.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

5.3.1 Manunuzi ya mali na vifaa ambavyo havikupokelewa Sh. 50,275,000

Mapitio ya mfumo wa manunuzi na mapokezi ya mali na vifaa ulibaini udhaifu ufuatao; hapakuwepo ushindani wa bei, manunuzi kufanyika bila kufuata mpango, kutopokelewa kwa vifaa na vifaa kutoingizwa kwenye daftari. Udhaifu huu ulionekana kwa Halmashauri kumi(10) na umewekwa wazi katika barua zilizotolewa kwa Halmashauri husika. Mchanganuo wa Halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 52 hapa chini:-

Jedwali Na.52: Manunuzi ya mali na vifaa ambavyo havikupokelewa

Na	Halmashauri	Amount (Shs.)
1.	Monduli	2,100,000
2.	Muheza	3,329,000
3.	Kilwa	2,297,800
4.	Lindi	1,313,000
5.	Nachingwea	1,686,400
6.	Manispaa ya Dodoma	3,886,261
7.	Manispaa ya Kigoma/Ujiji	12,004,000
8	Ngara	4,757,566
9	Mtwara	5,925,203
10	Chunya	10,575,000.
	Jumla	47,874,230

5.3.2 Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Kamati ya Uongozi wa Jamii (CMC) Sh.5,880,500

Manunuzi yenye thamani ya Sh.5,880,500 yalilipwa kwa mafundi kupitia akaunti ya kuongeza uwezo kwa miradi inayotekelezwa vijijini bila idhini ya wana kamati(CMC).Hii ni kinyume na aya 8.3.1 ya muongozo wa kazi TASAF II (Operational manual)

5.3.3 Mchanganuo wa gharama za kazi za ujenzi wenye thamani ya Sh.76,512,794.58 hazikuwasilishwa

Maeneo ya miradi sita ya manispaa ya Kigoma yalitembelewa kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa miradi and kuthibitisha kama ujenzi ulizingatia Mchanganuo wa gharama za kazi za ujenzi ulioidhinisha.Katika miradi tuliyotembelea hatupatiwa mchanganuo huo hivyo ilituwia vigumu kuthibitisha kama kazi ilifanyika kama ilivyotakiwa.Orodha ya miradi imeorodheshwa kwenye kwenye jedwali na.53 hapo chini:

Jedwali Na.53 Halmashauri haikuwasilishaMchanganuo wa gharama za kazi

Na	Eneo	Jina la mradi	Kiasi(Sh.)
1	MGEO	Ujenzi wa madarasa matatu (3) katika Busanda	11,507,691.68

2	BUSHABANI	Ujenzi matatu madarasa	10,545,370.18
3	KANDORO	Ujenzi matatu madarasa	12,541,875.18
4	NDARABU	Ujenzi matatu madarasa mawili Kirungu	11,750,479.68
5	MATOFARINI	Ujenzi matatu madarasa Kisingirma	14,555,330.68
6	KALAMATA	Ujenzi matatu madarasa	15,612,047.18
	Jumla		76,512,794.58

5.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

5.4.1 Miradi ambayo haikutekelezwa

Kulikuwa na miradi yenye thamani ya kiasi cha Sh.24,282,959,694 inayohusu Halmashauri arobaini na moja (41) ambayo haikutekelezwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha kama inavyoonekana kwenye jedwali namba. 54 hapa chini:

Jedwali Na. 54: Miradi ambayo haikutekelezwa

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala	441,000,000
2	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke	326,569,718
3	Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo	401,544,594
4	Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba	306,054,672
5	Halmashauri ya Wilaya ya Chato	76,752,043
6	Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi	524,818,307
7	Halmashauri ya Wilaya ya Bunda	1,630,652,415
8	Halmashauri ya Wilaya ya Musoma	1,022,585,205
9	Halmashauri ya Wilaya ya Rorya	1,597,077,838
10	Halmashauri ya Wilaya ya Geita	1,548,967,000
11	Halmashauri ya Wilaya ya Kahama	1,557,794,381
12	Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu	1,212,898,200
13	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	499,621,681
14	Halmashauri ya Wilaya ya Moshi	459,405,743
15	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	294,379,469
16	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi	381,334,945
17	Halmashauri ya Wilaya ya Njombe	193,828,601
18	Halmashauri ya Wilaya ya Ileje	591,104,734

19	Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	285,770,200
20	Halmashauri ya Manispaa ya Mbarali	4,800,000
21	Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya	1,050,938,221
22	Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi	1,304,540,664
23	Halmashauri ya Mji wa Mpanda	1,147,272,421
24	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	166,000,000
25	Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga	583,451,000
26	Halmashauri ya Wilaya ya Lindi	476,420,042
27	Halmashauri ya Wilaya ya Liwale	349,910,116
28	Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa	376,527,197
29	Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	675,836,907
30	Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	688,422,800
31	Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara	310,053,000
32	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu	567,987,740
33	Halmashauri ya Wilaya ya Newala	606,914,000
34	Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba	697,979,299
35	Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo	447,831,183
36	Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha	456,317,330
37	Halmashauri ya Mji wa Kabaha	269,441,118
38	Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga	482,745,009
39	Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji	916,763,947
40	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	207,246,129
41	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	356,300,024
	Jumla	24,282,959,694

5.4.2 Miradi ambayo haijatekelezwa/iliyoahirishwa au kuchelewa kukamilika katika Halmashauri, Sh. 10,880,651,475

Wakati wa ukaguzi miradi ya kiasi cha Sh. 10,880,651,475 ilikuwa haijatekelezwa au kukamilishwa na Halmashauri thelasini (30) mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2011/2012 kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali Na. 55 hapa chini:

Jedwali Na.55: Miradi ambayo haikutekelezwa kwa wakati uliokubalika

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	760,741,341
2	Halmashauri ya Manispaa ya	

	Kinondoni	305,459,000
3	Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo	207,741,385
4	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	456,770,500
5	Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe	158,612,997
6	Halmashauri ya Wilaya ya Tarime	79,280,000
7	Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe	229,975,400
8	Halmashauri ya Wilaya ya Maswa	422,207,300
9	Halmashauri ya Wilaya ya Meatu	299,827,000
10	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	748,552,785
11	Halmashauri ya Wilaya ya Siha	152,990,000
12	Halmashauri ya Wilaya ya Muheza	25,612,000
13	Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo	796,780,545
14	Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi	744,275,590
15	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe	935,769,500
16	Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda	988,558,830
17	Halmashauri ya Mji wa Mpanda	907,982,835
18	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	592,216,625
19	Halmashauri ya Wilaya ya Lindi	123,000,000
20	Halmashauri ya Manispaa ya Lindi	211,769,511
21	Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	265,881,656
22	Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	379,742,200

23	Halmashauri ya Manjspa ya Mtwara	213,768,160
24	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu	86,288,121
25	Halmashauri ya Wilaya ya Newala	68,517,145
26	Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba	109,842,032
27	Halmashauri ya Mji wa Kabaha	272,515,437
28	Halmashauri ya Wilaya ya Mafia	151,599,989
29	Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero	162,896,147
30	Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro	47,089,444
	Jumla	10,880,651,475

5.4.3.1 Vifaa vya thamani ya Sh. 28,595,049 Havijaingizwa kwenye vitabu

Vifaa vya thamani ya Sh.28,595,049 vilivyounuliwa na Halmashauri nane (8) viligundulika kutoingizwa kwenye vitabu husika vya Halmashauri husika. Maelezo zaidi yamo kwenye Jedwali Na.56 hapa chini:

Jedwali 56: Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye vitabu

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	9,135,000
2	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	5,072,000
3	Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi	3,566,000
4	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	3,744,000
5	Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga	4,305,000
6	Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi	667,000
7	Halmashauri ya Wilaya ya Ileje	2,106,049

8	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	12, 331,044
	Jumla	28,595,049

5.4.4 Vifaa vilivyonunuliwa bila bei shindani, Sh.9,925,899

Ukaguzi ulibaini vifaa vyenye thamani ya jumla ya kiasi cha Sh.9, 925,899 vilivyo nunuliwa na Halmashauri nne (4) kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali namba 57 ambavyo vilinunuliwa bila bei shindani kinyume na Kanuni namba 28 ya Kanuni za Umma za Ununuzi za mwaka 2005 pamoja na Jedwali la Kwanza la Kanuni zinazoongoza taratibu za Tenda katika Halmashauri za mwaka 2007.

Jedwali 57: Vifaa vilivyonunuliwa bila bei shindani

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe	2,000,000
2	Halmashauri ya Wilaya ya Babati	6,408,199
3	Halmashauri ya Mji wa Babati	833,250
4	Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi	684,450
	Jumla	9,925,899

5.4.5 Manunuzi kutoka kwa wasambazaji wasioidhinishwa, Sh.21,825,815

Ukaguzi ulibaini vifaa vyenye jumla ya Sh. vilivyonunuliwa na Halmashauri tatu (3) kutoka kwa wasambazaji ambao hawakuidhinishwa na Halmashauri husika kwa ajili ya usambazaji wa vifaa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kinyume na Kanuni Na.40 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2005. Maelezo zaidi yameonyeshwa kwenye jedwali namba 58 hapa chini:

Jedwali 58: Manunuzi kutoka kwa wasambazaji wasioidhinishwa

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Kondo	11,825,815

2	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	6,250,000
3	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	3,750,000
	Jumla	21,825,815

5.5 Miradi mingine

Mfuko wa kimataifa wa kupambana na ukimwi, Malaria, kifua kikuu na Ukoma

Jedwali 59: Miradi mingine dosari katika manunuzi

1	Health Systems Strengthening Global Fund Round 9 (HSSGFR9)
	<ul style="list-style-type: none"> Kukosekana kwa kumbukumbu za mikataba katika rejista ya mikataba Kumbukumbu za mikataba zenye malipo ya kiasi cha Shs. 299,026,000 kuhusu uimarishaji wa mfumo wa Afya mzunguko wa tisa (90) haikuonyeshwa katika rejista ya mikataba
2	National Aids Control Programme Global Fund Round 8 (NACPGFR8)
	<ul style="list-style-type: none"> Kutowasilishwa mpango wa manunuzi wa mwaka kwa ajili program ya kitaifa ya kudhibiti UKIMWI Kulikuwa na dosari katika manunuzi ya vifaa na huduma kiasi cha Sh. 72,127,368 Kutohibitishwa mapokezi ya vifaa vyenye thamani ya Sh.8,784,480

5.5.1 Miradi mingine isipokuwa Mfuko wa Kimataifa wa kupambana na UKIMWI Malaria Kifua Kikuu na Ukoma

1	Dar Rapid Transit Agency
	<ul style="list-style-type: none"> Wakala ilitoa kazi ya Ujenzi na Ulinzi ya thamani ya kiasi cha Sh. 111,027,970 bila idhini ya bodi ya zabuni na wala hapakuwepo mikataba
2	Transport Sector Support Project (TSSP), IDA Credit No.4724 - TZ and Credit No. 4991-TZ
	Tozo ya riba kwa kuchelewa kulipa hati za madai kwa wakati zenye thamani ya Sh. 19,053,525.36
3	TZ-Strategic Cities Project

	<p>Halmashauri ya Jiji Mwanza</p> <ul style="list-style-type: none"> • Vifaa vyenye thamani ya Sh 144,371,648.00 havikuingizwa daftarini • Manunuzi kiasi cha Sh. 11,600,000.00 yaliyofanyika bila ushindani <p>Halmashauri ya Jiji Mbeya</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kompyuta/mpakato za thamani ya Sh 42,376,700 zilinunuliwa bila alama za utambuzi wa kitaalamu Halmashauri ya Jiji Tanga • Manunuzi ya kiasi cha Sh.13,654,392bila ushindani <p>Halmashauri ya Manispaa Mtwara</p> <ul style="list-style-type: none"> • Manunuzi ya kiasi cha Sh.221,495,020bila ushindani
4	The Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative (TEITI)
	Mali za thamani ya kiasi cha Sh.18,381,242 zilionunuliwa hazikupewa alama za utambuzi .Pia, TEITI haitunzi kadi ya mali katika ofisi.
5	TZ-Marine & Costal Env Mgmt SIL (FY06) -TZ Mainland & Zanzibar (MACEMP)
	<ul style="list-style-type: none"> • Vifaa vya thamani ya Sh.19,360,000 vilitolewa bila kupokelewa na hati ya kutolea vifaa haikuwa imesainiwa na aliyepokea • Samani za kiasi cha Sh.32,930,000 hazikuletwa na wazabuni ingawa walishalipwa.
6	Mradi wa Rasilimali/Kitegauchumi Sekta ya Kilimo Wilayani -DASIP
	<ul style="list-style-type: none"> • Kitengo cha kuratibu miradi kilipanga kununua vitu mbalimbali kulingana na bajeti na mpango wa manunuzi. Hata hivyo, hadi Septemba 2012 manunuzi ya kiasi cha Sh.8,690,000,000yalikuwa bado hayajafanyika.
8	Miradi wa Kasi yaUsalama wa Chakula
	<p>Halmashauri ya Wilaya Sengereme</p> <ul style="list-style-type: none"> • Vocha za pembejeo za kiasi cha Sh. 1,755,542,000 zilipokelewa lakini hazijaandikwa kwenye leja husika.
9	Mradi wa Sayansi na Teknolojia Elimu ya Juu (STHEP)
	<ul style="list-style-type: none"> • Menejimenti ya COSTECH ilinunua jenereta mpya lenye uwezo wa 200KV kutoka INCA TANZANIA LTD kwa gharama ya kiasi cha dola za kimarekani 58,797.88. Mzabuni alilipwa kabla ya kufanya ukaguzi matokeo yake jenereta iliyoletwa haikuwa kama ilivyoainishwa kiufundi.

	<ul style="list-style-type: none"> Hakuna maelezo ya vifaa vya thamani ya Dola za Kimarekani 470,045.67
10	Wizara ya Elimu na Mafunzo-Zanzibar (UNDP)
	Wizara ilinunua vifaa vya thamani Sh.20,344,960 lakini havikuandikwa kwenye leja ya stoo kinyume na Kanuni ya 198 ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha mwaka 2004)
11	Ofisi ya Taifa ya Takwimu - NBS (UNDP)
	<p>Menejimenti ilikuwa na mkataba na Chuo Kikuu cha Ardhi kuorodhesha maeneo na ramani za usimamaizi katika mkoa wa Morogoro. Mkataba ulitakiwa kuanza tarehe 29 Januari, 2011 na kumalizika tarehe 29 Machi 2011. Malipo ya awali yalikuwa kiasi cha Sh. 46,851,971 kupitia hundi namba 631318. Ukaguzi ulibaini dosari zifuatazo:</p> <ul style="list-style-type: none"> Huduma za ushauri ulipatikana pasipo ushindani kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005. Utekelezaji wa mkataba haujakamilika na hakuna hatua zilizochukuliwa na uongozi kuhakikisha kuwa mshauri anakamilisha kazi.
12	The Marine and Coastal Environment Management Project - Global Environmental Facility (MACEMP - GEF)
	<ul style="list-style-type: none"> Mikataba haikusambazwa kwa mamlaka husika kkulinga na sheria Rejista ya mikataba haitunzwi Mapungufu katika kusimamia manunuzi ya kiasi cha Sh.53,595,600
13	The Marine and Coastal Environmental Management Project (MACEMP - IDA CREDIT NO 4106)
	<ul style="list-style-type: none"> Rejista ya mikataba haitunzwi Ujenzi wa Mvuvi House haujakamilika Malipo zaidi ya kiasi cha Sh.334,622,697 Kulikuwa na malipo mara mbili ya kiasi cha Sh.34,064,950

SURA YA SITA

UDHAIFU KATIKA USIMAMIZI WA FEDHA

6.0 Utangulizi

Sura hii inalenga kutoa upungufu uliobainika katika kusimamia fedha za miradi ya maendeleo uliotokana na ukaguzi. Hii inaangalia jinsi menejimenti ilivyoyashughulikia masuala yaliyoibuliwa katika ripoti zilizotangulia na masuala yaliyoibuliwa kwa mwaka huu wa fedha na jinsi mapendekezo yaliyotolewa yalivyofanyiwa kazi.

Madhumuni ya matokeo na mapendekezo ya ukaguzi ni kumsaidia mkaguliwa kufanya maboresho katika usimamizi wa fedha na kudhibiti rasilimali za taasisi. Kutokushughulikia matokeo na mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye taarifa kwa upande wa miradi iliyokaguliwa ina madhara makubwa sana kwa afisa masuuli na uongozi wa miradi.

Matatizoya kutoshughulikia matokeo na mapendekezo ya ukaguzi yanaweza kusababisha mapungufu yaliyoainishwa na ukaguzi kujirudia kwa miaka inayokuja. Hii inaweza kumaanisha kuwa afisa masuuli na uongozi hautoi uzito wa kutosha katika kushughulikia matatizo haya. Orodha ya mapungufu yaliyotolewa miaka ya nyuma ambayo hayajashughulikiwa na mapungufu yaliyojitokeza kuhusu usimamizi wa fedha za miradi yameonyeshwa hapa chini kwa kila mradi.

6.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)

6.1.1 Utekelezaji wa mapendekezo katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma

Halmashauri nyingi zimefanya vizuri katika kuyashughulikia na kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa miaka ya nyuma. Katika ukaguzi wa mwaka huu, Halmashauri 64 zilikuwa na masuala ya miaka ya nyuma yenye thamani ya Sh. 9,086,703,965.97 ambayo hayajatekelezwa (Angalia Kiambatisho IV).

6.1.2 Ucheleweshaji wa kuhamisha fedha kwenye akaunti za utekelezaji

Mara kadhaa kumekuwa na uchelewaji wa kuhamisha fedha kutoka akaunti kuu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwenda kwenye akaunti za watekelezaji. Fedha zinapoingia kwenye akaunti kuu, zinatakiwa kuhamishiwa mara moja kwenye akaunti ya Halmashauri. Hata hivyo hii hua haitokei.

6.1.3 Malipo yasiyokubalika Sh. 1,036,474,688.62

Halmashauri therathini na saba (37) zilifanya malipo ya kiasi cha Sh. 1,036,474,688.62 ambayo yalilipwa bila kuwa na nyaraka halisi ili kuthibitisha uhalali wa gharama husika. Halmashauri sita (6) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh.126,622,475.62 yaliyokuwa na kodi ya ongezeko la thamani, Halmashauri ishirini na saba (27) zilizohamisha kiasi cha Sh.605,135,500 kutoka kwenye akaunti ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Halmashauri kumi na sita (16) zilitumia kiasi cha Sh.299,206,506 kwenye shughuli zisizohusiana na mradi.

Mchanganuo wa malipo yasiyokubalika yameonyeshwa katika jedwali namba. 60 na maelezo ya kina katika **kiambatisho VII**.

Jedwali52: Malipoyasiyokubalika

Maelezo	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
Kodi la ongezeko la thamani	6	126,622,745.62
Mkopo isiyorejeshwa	4	5,509,936.00
Fedha zilizotumika kwa kazi zisizokuwa za mradi.	11	605,135,500.00
Matumizi ambayo hayakuwa kwenye bajeti	16	299,206,507.00
Jumla	37	1,036,474,688.62

6.1.4 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 394,055,695.50


Kulikuwa na malipo ya Sh. 394,055,695.50 yenye nyaraka pungufu. Kati ya kiasi hiki, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilikuwa na sehemu kubwa ya asilimia 12, ikifuatiwa na Halmashauri ya wilaya ya Arusha yenye asilimia 12.13 na Nachingwea ni ya tatu kwa kuwa na asilimia 8.78. Angalia kiambatisho namba VIII.

6.1.5 Hati za malipo zisizokaguliwa Sh.320,062,215

Hati za malipo (vocha) za thamani ya Sh. 320,062,215 zilizoandikwa kwenye daftari la fedha hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi. Hii ni kinyume na Kifungu 45(5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Halmashauri tisa (9) zilionekana kuwa na matumizi yasiyokuwa na hati za malipo, ikiongozwa na Mbarali iliyokuwa na asilimia 74, ikifuatiwa na Bunda yenye asilimia 8.73 na ya tatu ni Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo yenye asilimia 4. Usahihi na uhalali wa malipo yaliyofanyika haukuweza kuthibitishwa kwa kukosekana kwa nyaraka na imepunguza mawanda ya ukaguzi.

6.1.6 Masurufu yasiyorejeshwa Sh. 75,916,237

Masurufu yenye jumla ya Sh. 75,916,237 kwenye halmashauri kumi na sita (16) hayakurejeshwa baada ya kazi iliyokusudiwa kukamilika baadhi ya maafisa ambayo hawakurejesha masurufu yao ya awali, walipatiwa masurufu mengine kinyume na Agizo namba 134 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (1997), linalotaka masurufu yanayotolewa kurejeshwa mara moja baada ya shughuli iliyokusudiwa inapokamilika. Kadhalika inazuia mtu mwenye masurufu yasiyorejeshwa kupatiwa mengine hadi hapo atakapokwisha rejesha yale ya mwanzo. Ukaguzi wa hesabu ulionyesha kuwa Halmashauri kumi na sita (16) zilikuwa na masurufu yasiyorejeshwa mwisho wa mwaka kama ilivyoonyeshwa katika kiambatisho namba IX.



6.1.7 Fedha zilizosalia bila kutumika Sh. 32,237,919,190.67

Wizara ya fedha ina akaunti kuu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ambayo inatunza fedha kabla haijazihamishia kwenye akaunti za watekelezaji mbalimbali. Ukaguzi ulibaini kiasi cha Sh. 32,237,919,190.67 cha miaka ya nyuma kilikuwa kwenye akaunti za Halmashauri. Fedha hizo zilitolewa katika mwaka wa fedha 2011/2012 lakini zilikuwa hazijatumika na sababu kuwalikuwa na ucheleweshwaji wa kuhamisha fedha, fedha hizo kukosa matumizi na utaratibu mrefu kwa manunuzi yanayohitaji mikataba. Pia ilibainika kuwa kulikuwa na miradi yenye thamani ya Sh. 3,937,196,386.54 iliyokuwa kwenye bajeti lakini haikutekelezwa kwa sababu ilikuwa inasubiri fedha imeonyeshwa katika kiambatisho namba III. Miradi ambayo haijatekelezwa inaendelea kuwa na madhara katika utendaji wa Halmashauri.

6.2 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

6.2.1 Mapitio ya utekelezaji wa mapendekezo ya wakaguzi kuhusu masuala ya miaka ya nyuma

Mapitio ya utekelezaji wa masuala yaliyoibuliwa katika kaguzi za miaka iliyopita na hasa mambo yaliyoonyesha kasoro, yalionyesha kuwa mambo mengi yamefanyiwa kazi isipokuwa

masuala yenye thamani ya Sh. 220,078,175 kama ilivyoonyeshwa katika jedwali namba 61 hapa chini:

Jedwali 61: Mapendekezo ambayo hayakutekelezwa

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	4,551,500
2	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	38,010,450
3	Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge	14,963,580
4	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	3,440,000
5	Halmashauri ya Manispaa ya Arusha	19,933,775
6	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	1,580,000
7	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	11,742,500
8	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	2,370,000
9	Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga	2,599,000
10	Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo	97,091,000
11	Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea	12,894,910
12	Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara	1,040,000
13	Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero	5,946,000
14	Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro	3,915,460
	Jumla	220,078,175

6.2.2 Malipo yasiyokubalika Sh.353,036,793

Malipo yasiyokubalika ya jumla ya kiasi cha Sh.353,036,793 yalifanywa na Halmashauri kumi (10) kwa manufaa yasiyokuwa ya mradi kinyume na makubaliano kati

ya Serikali ya Tanzania na Wadau wa Maendeleo kifungu namba 9.2.2 kinachozuia ulipaji kodi kutoka kwenye fedha za mradi. Jedwali namba 62 hapa chini linaonyesha Halmashauri zilizofanya malipo yasiyokubalika:

Jedwali 62: Malipo yasiyokubalika

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Iramba	202,500
2	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	322,488
3	Halmashauri ya Wilaya ya Singida	342,000
4	Halmashauri ya Wilaya ya Magu	64,477,295
5	Halmashauri ya Jiji la Mwanza	69,208,165
6	Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe	4,080,000
7	Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe	1,091,825
8	Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo	77,502,520
9	Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali	133,321,000
10	Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga	2,489,000
	Jumla	353,036,793

6.2.3 Masurufu yasiyorejeshwa, Sh. 5,273,600

Kulikuwa na masurufu ya jumla ya kiasi cha Sh.5,273,600 yanayohusu Halmashauri nne (4) (ambazo zimeodhoresha katika jedwali namba 63 hapa chini) yaliyotolewa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hata hivyo yalionekana kutorejeshwa mpaka mwisho wa mwaka kinyume na Agizo na. 134 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (1997).

Jedwali 63: Masurufu yasiyorejeshwa

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma	1,353,000
2	Halmashauri ya Manispaa ya Arusha	911,000
3	Halmashauri ya Wilaya ya Chunya	1,875,000
4	Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe	1,134,600
	Jumla	5,273,600

6.2.4 Malipo yenye nyaraka pungufu, Sh.421, 637,516

Kulikuwa na malipo yenye nyaraka pungufu ya jumla ya kiasi cha Sh. 421,637,516 yaliyofanywa kinyume na kifungu namba 45 (5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 pamoja na Agizo namba 8(2)(c) Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (2009). Maelezo zaidi yameonyeshwa kwenye jedwali namba 64 hapa chini:

Jedwali 64: Malipo yenye nyaraka pungufu

S/N	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	1,960,000
2	Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa	6,370,000
3	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapa	225,000
4	Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge	68,252,810
5	Halmashauri ya Wilaya ya Tabora	2,900,000
6	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	8,200,000
7	Halmashauri ya Wilaya ya Rorya	9,527,020
8	Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe	14,684,000
9	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	3,596,490
10	Halmashauri ya Manispaa ya Arusha	43,736,750
11	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	900,000
12	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	2,412,000
13	Halmashauri ya Wilaya ya Babati	349,000
14	Halmashauri ya Mji wa Babati	1,707,703
15	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto	450,000
16	Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe	61,768,001
17	Halmashauri ya Wilaya ya Chunya	58,443,852
18	Halmashauri ya Wilaya ya Ileje	6,571,000
19	Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga	2,839,000

20	Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo	27,478,000
21	Halmashauri ya Wilaya ya Songea	4,385,000
22	Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo	2,830,000
23	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	3,135,000
24	Halmashauri ya Wilaya ya Lindi DC	3,925,000
25	Halmashauri ya Manispaa ya Lindi	630,900
26	Halmashauri ya Wilaya ya Liwale	59,497,938
27	Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea	4,525,000
28	Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero	18,218,500
29	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	2,119,552
	Jumla	421,637,516

6.2.6 Upungufu wa wataalamu katika Idara ya Maji katika Halmashauri

Ukaguzi ulibaini upungufu wa wataalamu wa maji katika Idara za maji katika Halmashauri nyingi nchini na hii imeathiri utekelezaji na usimamiaji wa miradi ya maji katika Halmashauri. Ukaguzi uliofanyika katika Halmashauri ishirini na nne (24) ulionyesha upungufu wa wataalamu wa maji kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali namba 65 hapa chini:

Jedwali 65: Upungufu wa wataalamu katika Idara ya Maji

Halmashauri	Wahandisi wa Maji		Mafundi wenye vyeti (FTC)		Mafundi Mchundo	
	Wanaotakiwa	Waliopo	Wanaotakiwa	Waliopo	Wanaotakiwa	Waliopo
Wilaya ya Rombo	5	1	9	2	10	4
Wilaya ya Mwanga	2	1	6	1	8	13
Manispaa ya Moshi	1	1	2	1	0	0

Wilaya ya Korogwe	5	2	18	12	1	0
Wilaya ya Muheza	3	1	10	2	12	2
Wilaya ya Kiteto	2	1	17	9	0	0
Wilaya ya Bukoba	3	0	8	0	0	4
Wilaya ya Missenyi	4	1	10	2	4	2
Karagwe Dc	5	1	39	14	10	8
Maswa Dc	1	1	6	5	0	0
Wilaya ya Kahama	2	2	20	8	5	4
Wilaya ya Kondo	2	0	11	6	0	0
Wilaya ya Manyoni	4	1	3	0	9	2
Wilaya ya Singida	4	1	8	0	0	2
Manispaa ya Singida	1	1	2	0	1	0
Wilaya ya Kigoma	4	1	10	1	10	4
Manispaa ya Kigoma/Ujiji	2	1	2	0		
Kibondo Dc	4	0	4	0	7	5
Wilaya ya Nzega	2	1	4	1	8	0
Wilaya ya Igunga	2	2	7	5	6	0
Manispaa ya Tabora	3	1	6	0	6	0
Wilaya ya Serengeti	4	1	22	4	0	5
Wilaya ya Rorya	3	1	12	1	0	0
Wilaya ya Bunda	4	2	22	7	0	14
Jumla	72	25	258	81	27	24

6.3 Mfuko wa Maendeleo ya Afya

6.3.1 Mapitio ya masuala ya miaka ya nyuma

Mapitio ya utekelezaji wa masuala yaliyoainishwa katika ukaguzi wa miaka iliyopita na hasa mambo yaliyokuwa na kasoro, yalionyesha kuwa mambo mengi yamefanyiwa kazi isipokuwa masuala yenye thamani ya Sh.10,982,257,870.41 kama ilivyoonyeshwa katika kiambatisho namba X.

6.3.2 Fedha isiyotumika Sh. 12,405,750,901

